

FURSA KIBAO ZIARA YA RAIS SAMIA UTURUKI UK. 5


epaper.ippmedia.com
www.ippmedia.com
0745 700710
LIKE & FOLLOW US
Alhamisi Aprili 18, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

MWANGA WA JAMII
ISSN 0856 • Na. 0581650
nipasheTZ nipasheTZ
www.ippmedia.com
The Nipashe Digital
nipashedigital

# Rais Samia aidhinisha ajira mpya zaidi 46,000

> "Kati ya nafasi hizo 12,000 ni kwa ajili ya sekta ya elimu na zaidi ya 10,000 ni kada ya afya. Nafasi hizo zitapunguza kwa kiasi kikubwa uhaba wa watumishi.
>
> **Simbachawene**



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, George Simbachawene




Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akifungua mkutano wa mafunzo ya kuwajengea uwezo wajumbe na wataalamu wa kamati za usimamizi wa fedha za umma kwa nchi wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADCOPAC), Zanzibar jana. Kulia ni Katibu Mkuu Kiongozi Zanzibar, Mhandisi Zena Said. **PICHA: IKULU**

**Watanzania** wengi 'mabonge' kisa kutokuzingatia ulaji unaofaa UKURASA 2





**Mbunge** ataka kauli 'magofu' kutoendelezwa kwa ujenzi Dar UKURASA 3

**Kinana** aonya viongozi kutoa ahadi 'hewa' UKURASA 3



# Mbunge Msukuma adai kikokotoo mafao chanzo watumishi wezi

UKURASA 7



# Dk. Mwinyi mapambano ya rushwa yanachochea maendeleo

UKURASA 17

**MICHEZO** PACOME FITI 100% KUITUMIKIA YANGA UK.24

**KATUNI** UK.6

HABARI KITAIFA



Katibu Mkuu Wizara ya Mambo ya Ndani, Ally Gugu (wa pili kulia), akimsikiliza Kamishna Jenerali wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, John Masunga baada ya kukagua mradi wa ujenzi wa majengo sita ya nyumba za askari wa jeshi hilo, ambayo yamekamilika, katika eneo la Kikombo, jijini Dodoma jana, ambapo familia 60 zitanufaika na mradi huo. **PICHA: WMNN**

# Samia aidhinisha ajira mpya 46,000

**Na Vitus Audax,** DODOMA

WABUNGE wameitaka serikali kuja na mpango mkakati wa kutoa ajira za kutosha katika kada za elimu na afya ili kukabiliana na uhaba wa watumishi nchini hali itakayoendana na utekelezaji wa miundombinu uliofanyika hivi karibuni.

Wakichangia makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kwa mwaka 2024/25, walisema sekta hizo zinahitaji ajira za kutosha.

Aidha, baada ya wabunge wanne kuchangia hoja ya ajira, Waziri wa Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, George Simbachawene alilijulisha Bunge kuwa usiku wa kuamkia jana Rais Samia Suluhu Hassan, alisikia kilio chao na kutoa kibali cha ajira 46,000 kwa kada mbalimbali.

Mbunge wa Nkasi Kaskazini (CHADEMA), Aida Khenani, alisema uboreshaji na ujenzi wa miundombinu ya shule pamoja na sekta ya afya vinatakiwa kuendana na ongezeko la watumishi kwa serikali kutoa ajira za kutosha ili majengo husika yaweze kutumika ipasavyo kwa maslahi ya wananchi.

Alisema kwa sasa serikali ijikite zaidi kupeleka watumishi pamoja na vifaa tiba katika vituo vinavyojengwa, alitaja katika jimbo lake wana upungufu wa walimu shule 175, sekondari upungufu walimu 202, afya watumishi 175.

"Natambua kwamba kuna ujenzi wa madarasa, vituo vya afya pamoja na zahanati kote nchini, lakini jambo hili litakuwa na maana zaidi kama tunaongeza idadi ya madarasa, lazima iendane na idadi ya walimu kwani shida ya Watanzania sio majengo bali ni elimu na huduma bora za afya," alisema Khenani.

Aidha, alitaja upungufu wa watumishi wengine wanaotegemewa zaidi katika maeneo husika ni pamoja na watumishi saba, watendaji 15 hali inayorudisha nyuma ukusanyaji mapato, watendaji wa vijiji ni 25.

Mbunge wa Nanyamba (CCM) Abdallah Chikota alitaja uhaba wa watumishi katika jimbo lake kuwa mkubwa hali inayoathiri utoaji huduma kwa wananchi.

Alipendekeza katika suala hilo waitazame zaidi mikoa ya pembeni kama Mtwara ambako kuna uhitaji wa watumishi sekta ya afya 6,088 na waliopo ni 2,153 pekee, aliiomba TAMISEMI kuomba kibali kwa ajili ya kutoa ajira.

Mbunge wa Urambo (CCM), Margaret Sitta alisema suala uhaba wa wafanyakazi kwa sasa ni kubwa katika maeneo mbalimbali na kutaja wilayani kwake kuwa wilaya nzima ina madaktari wanne pekee wakiwa na uhaba wa madaktari 18.

"Hao ni madaktari tu hatujazungumzia kuhusu wahudumu wengine wakiwamo wauguzi, serikali ije na mpango mkakati wa kuongeza watumishi, ikiwa ni pamoja na kada ya walimu yenye uhitaji mkubwa pia," alisema Sitta.

Mbunge wa Katavi (CCM), Martha Mariki, alisema fedha zilizotumika katika uboreshaji wa miundombinu ya majengo ya shule na afya mkoani kwake wana uhaba wa watumishi kwa sekta ya afya kwa zaidi ya asilimia 57 hali inayosababisha fedha zilizotumika kutokuonekana kazi yake.

**AJIRA 46,000**

Waziri Simbachawene alisema nafasi hizo 12,000 ni kwaajili ya sekta ya elimu na zaidi ya 10,000 ni kwa upande wa kada ya afya, fursa hizo zitapunguza kwa kiasi kikubwa changamoto ya watumishi kama zilivyotolewa na wabunge.

Akiwasilisha makadirio ya wizara ya OR-TAMISEMI, Mohammed Mchengerwa alisema wizara hiyo itawezesha upatikanaji wa watumishi 400 wa mkataba watakaofanya kazi katika vituo vya kutolea huduma za afya, kulipa mishahara kwa watumishi 400 watakaoajiriwa. Naibu Waziri, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Ridhiwani Kikwete, alisema kwa mwaka 2023/24 serikali ilitoa nafasi za ajira kada ya walimu 10,505 huku kwa mwaka 2024/25, inatarajia kutoa ajira mpya kwa walimu 10,590 ili kutatua kwa kiwango kikubwa kero zilizopo katika eneo hilo.

Naibu Spika, Mussa Zungu, aliitaka serikali wakati wa kutoa fursa hizo za ajira kutoa ajira kwa walimu wanaojitolea kwa zaidi ya miaka mitatu hadi minne kwa kuwa wameonesha moyo wa kuisaidia serikali kwa muda mrefu.

# Tanzania wengi mabonge kisa kutokuzingatia ulaji unaofaa

**Na Restuta James**

WATANZANIA wengi wana uzito uliopitiliza (mabonge) kutokana na kutozingatia ulaji unaofaa huku takwimu zikionyesha ni watu saba pekee nchini katika 100 wanaozingatia mlo kamili.

Takwimu zinaonyesha Mtanzania mmoja katika watatu, ana uzito uliokithiri na watu wenye elimu na uhakika wa kipato ndio waathirika zaidi.

Mkurugenzi Msaidizi wa Magonjwa Yasiyoambukiza (NCD) katika Wizara ya Afya, Dk. Omary Ubuguyu, aliyasema hayo jana Dar es Salaam wakati wa kongamano la kwanza la uimara wa afya kwa ajili ya biashara endelevu, lililoandaliwa na Mtandao wa Global Compact Tanzania (GCNT) na kukutanisha wadau wa sekta binafsi.

"Katika maeneo machache ambayo tunafanya vizuri ni kwenye mazoezi kwa sababu kumekuwa kwa mfano marathoni nyingi hatufanyi vizuri kabisa katika masuala ya ulaji bado ni watu saba katika 100 ambao wanazingatia ulaji unaofaa.

"Suala la uzito na unene kupita kiasi pia hali imezidi kuwa mbaya, zamani ilikuwa ni katika kila watu wanne, mmoja anauzito uliokithiri, sasa hivi ni mtu mmoja katika kila watu watatu ana uzito au unene uliokithiri, kwa hiyo hatufanyi vizuri katika eneo hili," alisema.

Dk. Ubuguyu alisema idadi ya watu ambao wanatumia pombe nchini imepungua lakini matumizi yameongezeka.

"Bahati mbaya kuliko zote vijana wanaathirika zaidi kuliko rika lingine lolote na wanawake wanaathirika zaidi kuliko wanaume katika haya tunayoyazungumza. Watu wenye umri mdogo na wanawake ndio wako kwenye hatari zaidi,' alisema.

Alisema utafiti unaonyesha kwamba magonjwa yasiyoambukiza kama saratani, kisukari, figo na shinikizo la juu la damu, yanaathiri zaidi watu wenye kipato cha chini, lakini ni kinyume chake katika baadhi ya nchi kama Tanzania ambako waathirika wakubwa ni wasomi na wenye uhakika wa kipato.

"Katika jamii mfano za wafanyakazi ndio wanaotumia vyakula vya viwandani zaidi, pombe zaidi, ndio watu wenye fursa ya kununua soda na vitu vingine ambavyo vinaathiri afya," alisema.

Dk. Ubuguyu alisema wafanyakazi wanaathirika zaidi kutokana na mtindo wa maisha kwa kuwa hawana nafasi ya kupata chakula bora kwa kuwa wananunua vyakula wasivyojua namna vilivyoandaliwa na pia hawapati nafasi ya kufanya mazoezi.

Mkurugenzi Mtendaji wa Mtandao wa Global Compact Tanzania (GCNT), Mardha Macatta-Yambi, alizitaka kampuni binafsi na wawekezaji kuweka mazingira ya kuhakikisha afya za wafanyakazi ni nzuri, ili kukabili NCD.

Alisema wadau wote wanapaswa kuunganisha nguvu kwa kuwa ongezeko la magonjwa hayo linaathiri biashara na uchumi wa nchi.

"Pamoja na serikali kuweka sera na mikakati ya kukabili magonjwa haya, makampuni yana nafasi kubwa kuhakikisha kwamba wafanyakazi wanakuwa na uelewa wa kutosha kuhusu afya zao kwa kuwa hawa ndio nguvu kazi ya kuwatengenezea faida kwenye kile walichowekeza," alisema.

# Nyuki wazua taharuki, wajeruhi wanafunzi 17

**Na Thobias Mwanakatwe,** MANYONI

KUNDI la nyuki limevamia Shule Shikizi ya Mjiha, Manyoni mkoani Singida na kujeruhi wanafunzi 17 ambao walipelekwa katika Zahanati ya Kijiji cha Heka kwa ajili ya matibabu.

Tukio hilo lilitokea juzi wakati wanafunzi hao wakiwa darasani wakiendelea na masomo ndipo kundi la nyuki lilipovamia shule hiyo na kuanza kuwashambulia wanafunzi na walimu ambao kila mmoja alianza kukimbilia vichakani kujihami.

Mmoja wa walimu wa shule hiyo, Hadija Selemani, akizungunza wakati Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Manyoni, Jumanne Makhanda, alipotembelea kuwapa pole wanafunzi hao, alisema uvamizi wa nyuki hao ulizua taharuki kubwa na kuingilia shughuli za masomo.

"Nyuki walipovamia shule wanafunzi walianza kukimbia ovyo kwenda vichakani kunusuru maisha yao, lakini wakati huo wako ambao tayari walikuwa wamejeruhiwa kwa kung'atwa na nyuki hao," alisema.

Selemani alisema baada ya tukio hilo, wanakijiji walianza kupiga yowe na wengine kufika shuleni hapo kuokoa watoto na baada ya muda, kundi hilo la nyuki liliondoka katika mazingira ya shule.

Alisema wanafunzi 17 ambao walikuwa wamejeruhiwa walichukuliwa haraka na kupelekwa katika zahanati ya Heka kwa ajili ya matibabu.

Mwenyekiti Makhanda alifika katika zahanati ya Kijiji cha Heka kuwapa pole wanafunzi hao ambao walikuwa wakiendelea kutibiwa na kutoa pesa za kuwanunulia vinywaji na vitafunwa.

"Kwa niaba ya CCM nawapa pole sana kwa tukio hili na zahanati hii pamoja na kwamba ni ndogo lakini imeweza kuwahudumia wanafunzi hawa tumeambiwa na wahudumu dawa zipo watahudumiwa vizuri," alisema.

Makhanda alisema kama itatokea kuna mwanafunzi hali yake itakuwa mbaya zaidi, gari la CCM ambalo lililala katika Kijiji cha Heka litakuwa tayari kumchukua na kumpeleka katika Hospitali ya Wilaya ya Manyoni kwa matibabu zaidi.

Mwenyekiti huyo pia alisema wazazi wasilazimishe kuwachukua watoto wao kurudi nao nyumbani kama wanafunzi hao watakuwa hawajatibiwa na madaktari kujiridhisha kuwa wamepona.

## HABARI KITAIFA

# Kinana aonya viongozi kutoa ahadi 'hewa', Nchimbi awafariji wa maporomoko Mbeya

**Na Waandishi Wetu**

MAKAMU Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi (CCM) Bara, Abdulrahman Kinana, ameshauri viongozi wa serikali kuacha kuahidi mambo ambayo hayajawekewa mipango, au wasiyojua kuwa utekelezaji wake utafanyika lini ili kuepusha malalamiko yanayotolewa na wananchi.

Aidha, Katibu Mkuu wa CCM, Balozi Dk. Emmanuel Nchimbi, amewataka Watanzania kujituma na kufanyakazi kwa bidii huku wakiacha kujihusisha na vitendo vya kutoa na kupokea rushwa.

Balozi Nchimbi pia, aliwatembelea waathirika 50 wa mmomonyoko wa ardhi katika Mlima Kawetere, Kata ya Itezi jijini Mbeya na kuwakabidhi Sh. milioni 10.

Akizungumza na wananchi wilayani Bunda, mkoani Mara, Kinana alipokea malalamiko ya wananchi dhidi ya serikali kuwataka wahame katika maeneo yao kupisha ujenzi wa mradi wa maendeleo, ambao walidai kuwa hawajalipwa hadi sasa licha ya kufanyiwa tathmini muda mrefu.

Wananchi hao walionesha kukerwa na kitendo cha maeneo yao kuchukuliwa na nyumba zao kubomolewa pamoja na kupewa masharti ya kutofanya shughuli zozote za kimaendeleo katika maeneo hayo ikiwamo Kijiji cha Nyantwate.

"Viongozi wa serikali kabla ya kuwahamisha wananchi ni vyema wakaeleza ni lini ahadi hiyo itatekelezwa, kama ni watu kuhama watahama lini, na fidia watapewa lini, hakuna sababu ya kutoa ahadi halafu inakaa miaka na miaka, kila kiongozi anakuja anaahidi anaondoka."

Mwananchi wa kijiji cha Nyantwali, Saasita Mchanga, mmoja wa wanaohitaji kulipwa fidia baada ya kupisha mradi wa maendeleo, alisema wanateswa na ahadi hiyo huku akidai wanashindwa kujenga matundu ya vyoo kwenye shule iliyoko eneo hilo wakisubiri hatima yao ili wahame.

"Shule yetu vyoo vilishadondoka ukifika pale watoto zaidi ya 400 wanatumia labda matundu mawili, wananchi wa Nyantwali tunaomba kama bado hatujaondolewa basi turuhusiwe tufanye maendeleo kuwanusuru watoto wetu kwasababu kuna magonjwa ya milipuko," alisema Mchanga.

Kutokana na hali hiyo, Kinana aliwashauri watendaji wa serikali kabla ya maamuzi yanayohusu kuhamisha watu, kufidia au kufanya jambo lolote linaloigusa jamii, wafanye utafiti wa kutosha wawe na uhakika, fedha zipatikane ndio watoe kauli, badala ya kutanguliza kauli kabla ya kutangaza fidia.

Alibainisha kuwa kumekuwa na tabia kwa viongozi kuwaambia wananchi wahame au wasilime katika maeneo yao halafu hakuna kinachoendelea.

Aidha, alisema anakumbuka wananchi hao waliahidiwa na mwaka jana mawaziri sita walikwenda katika eneo hilo wakiwa na usafiri wa helikopta na kuwataka watu wahame.

"Sasa walitoa ahadi bila kujiandaa na wamedanganya watu, leo wananchi wanakuja kuniuliza mimi sasa nitawajibu nini? Nataka kuwasihi hapa watendaji wa serikali kabla kuahidi kitu ni muhimu mkaanza kwanza kujipanga kuepusha usumbufu.

"Kama alivyosema Rais Samia Suluhu Hassan wakati anawaapisha wakuu wa mikoa juzi, waende wahakikishe watu wanapewa haki yao, nitaongea na Waziri wa Fedha nimuulize vipi kuhusu malipo yenu aniambie kama imefika mwisho au bado," alisema Kinana.

Katika hatua nyingine, Dk. Nchimbi aliwataka wananchi kuendelea kuchapakazi kwa bidii, kufanyakazi zitakazowaingizia kipato kihalali na kujiepusha na rushwa kwa kuwa siku zote ndio adui wa haki.

"Kuchapa kazi ni kuendelea kuunga mkono juhudi za Rais Samia kuwataka Watanzania wote kufanyakazi na ndipo tutazidi kulijenga taifa letu na kuimarika kiuchumi."

Vile vile, alisema viongozi wa kitaifa wa CCM watendelea kuisimamia serikali kutimiza wajibu wake na kutekeleza ilani ya uchaguzi ya mwaka 2020/2025.

***Imeandikwa na Maulid Mmbaga (MARA) na Khalfan Chusi (Mbeya)**

# Mbunge ataka kauli 'magofu' kutokuendelezwa ujenzi Dar

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MBUNGE wa Kinondoni (CCM), Tarimba Abbas, ameitaka serikali itoe kauli kuhusu majengo ambayo ujenzi wake umesimama kwa muda mrefu jijini Dar es Salaam pamoja na kuweka sheria ya ukomo wa ujenzi.

Hata hivyo, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi imetoa rai watu ambao hawajakamilisha ujenzi wa majengo yao katika miji mbalimbali watumie utaratibu wa sera ya ubia ili kukamilisha ujenzi wa majengo hayo.

Akijibu swali la Mbunge huyo, Naibu Waziri wa Wizara hiyo, Geophrey Pinda alikiri kuwapo na baadhi ya majengo ambayo ujenzi umesimama kwa muda mrefu jijini humo na maeneo mengine nchini.

Alisema hali hiyo kwa kiasi kikubwa inasababishwa na baadhi ya waendelezaji kujenga majengo kwa kutumia fedha zao binafsi za kudunduliza hali inayosababisha kuchukua muda mrefu. "Katika kuwezesha upatikanaji mikopo ya nyumba nchini, Bunge lilitunga Sheria ya Mikopo ya Nyumba Na. 16 ya mwaka 2008, ili kuwezesha benki za biashara kutoa mikopo kwa ajili ya ujenzi na ununuzi wa nyumba," alisema.

Alifafanua kuwa mikopo katika benki hizo imekuwa na riba kubwa jambo ambalo linawafanya Watanzania wengi kushindwa kumudu mikopo hiyo pamoja na kusababisha gharama za nyumba zinazojengwa kuwa kubwa.

"Serikali imeendelea kuchukua hatua mbalimbali za kuhakikisha kuwa kunakuwepo mazingira wezeshi ya ujenzi wa majengo, ikiwa ni pamoja na kuhimiza ushindani katika sekta ya fedha ili kuwezesha kushuka kwa riba za mikopo ya nyumba mathalan kutoka asilimia 21 ya sasa hadi asilimia 12," alisema.

Nipashe The Guardian

Kutoka Menejimenti ya The Guardian Limited



**Wapendwa Wateja wetu**

Tunayo furaha kutangaza hatua kubwa kuelekea upatikanaji wa magazeti yetu kidijitali. Kuanzia tarehe 13 Aprili 2024, magazeti ya wikiendi ya **Nipashe Jumamosi, Nipashe Jumapili na The Guardian on Saturday** yanapatikana kwa njia ya gazeti-mtandao kupitia **epaper.ippmedia.com** au **www.ippmedia.com**

Siku za wiki (Jumatatu hadi Ijumaa) utaendelea kufurahia matoleo yote, kuchapishwa na Mtandaoni

Asante kwa usomaji wako, na kuendelea kuwa nasi katika mabadiliko haya.

Kwa mawasiliano zaidi Tupigie: 0677 020 701
Subscription: 0625 174 714
Barua pepe: customerrelations@guardian.co.tz

# PM aonya watoa misaada wachonganishi

**Na Julieth Mkireri,** RUFIJI

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, ameonya tabia ya baadhi ya wadau wanaotoa misaada kwa waathirika wa mafuriko Rufiji mkoani Pwani na kuwataka kuacha mara moja kupotosha na kuwachonganisha wananchi na serikali.

Akizungumza baada ya kutembelea waathirika hao juzi katika kambi ya Chumbi wilayani Rufiji, alisema suala la mafuriko ni kubwa na halipaswi kufanyiwa mzaha, hivyo tabia ya kuwachanganya na kuwapotosha wananchi juu ya chanzo chake si sahihi na serikali haiwezi kufumbia macho.

Baadhi ya wadau, alisema wamekuwa wakifika katika maeneo hayo na kutoa matamshi yanayoudhi kwamba chanzo cha mafuriko hayo ni ujenzi wa Bwawa la Kufua Umeme la Julius Nyerere, jambo ambalo si sahihi kutokana na ukweli kwamba eneo hilo limekuwa likikumbwa na mafuriko kwa

“Tunatambua michango na misaada inayotolewa na wadau mbalimbali lakini tunaomba msije kuwapotosha na kuwachanganya wananchi juu ya chanzo cha mafuriko. Nimetoka Morogoro mafuriko ni mengi. Je, pale pana bwawa? Mafuriko hapa yapo miaka yote na hali imekuwa hivi kutokana na wananchi kujenga mabondeni,” alisema. Pia alisema serikali kupitia kamati ya maafa kitaifa, iko kazini kuhakikisha waathirika wote wa mafuriko nchini wanapata huduma mbalimbali zikiwamo chakula, maji safi na afya pamoja na kuwatafutia maeneo salama kwa ajili ya makazi.

Waziri Mkuu alisema baadhi ya watu wasio waaminifu wamekuwa wakijichanganya na waathirika kwa lengo la kujipatia misaada mbalimba jambo ambalo si sahihi. Aliwaagiza watendaji wa vijiji na wenyeviti kuwatambua wananchi wao ili kuondoa mkanganyiko.

“Watendaji wa vijiji na kata mshirikiane na kamati hizi za maafa kuwatambua watu walioathirika ili tuache kuhudumia watu ambao hawajapata maafa na kuwawezesha wahusika kuhudumiwa na kunufaika na misaada hii,” alisema.

Pia aliziagiza serikali za vijiji katika maeneo yote yaliopata maafa nchini kutafuta maeneo mazuri yenye miinuko ili kuwahamishia wananchi katika maeneo hayo na kwamba maeneo ya mambondeni yatunike kwa kilimo na si makazi.

“Niwasihi wananchi mwendelee kusikiliza serikali na maelekezo tunayotoa mvua bado zipo na kila siku zinanyesha na Mamlaka ya Hali ya Hewa imesema mvua zipo mpaka mwezi Mei, hivyo walioko mabondeni waendelee kuchukua tahadhari ikiwamo kuondoka katika maeneo hayo,” alisema.

Majaliwa pia aliziagiza kamati za maafa kuhakikisha misaada yote inayotolewa na serikali na wadau mbalimbali inatumika kwa malengo yaliyokusudiwa sambamba na Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) na Wakala wa Barabara Vijijini (TARURA) kuimarisha miundombinu ya barabara.

Akitoa taarifa ya maendeleo ya waathirika hao, Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Abubakar Kunenge, alisema kwa sasa hali ni nzuri na kwamba wananchi wanaendelea kupata huduma mbalimbali ikiwemo za afya.

“Waathirika tulio nao hapa ni zaidi ya 2,880 na katika kambi hii, wako 411. Huduma zinaendelea kutolewa kama kawaida na misaada bado inahitajika. Naomba wadau waendelee kujitoleza,” alisema Kunenge.



Rais Samia Suluhu Hassan akisalimiana na wafanyabiashara mbalimbali pamoja na abiria aliosafiri nao kwenye ndege wakati akielekea jijini Ankara kwa ajili ya ziara rasmi nchini Uturuki. **PICHA: IKULU**

# Wabuge wataka TARURA iongezewe nguvu kukabili ubovu wa miundombinu

**Na Vitus Audax,** DODOMA

KUTOKANA na Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini (TARURA) kuwa na majukumu makubwa, wabunge wameitaka serikali kuipa nguvu zaidi kwa kuongeza fedha, rasilimali watu na kutochelewesha fedha za miradi.

Ombi hilo limetolewa na wabunge kwa nyakati tofauti wakati wakichangia makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kwa mwaka 2024/25.

Mbunge wa Nanyamba (CCM), Abdallah Chikota, alisema licha ya TARURA kuwa na miaka saba pekee tangu kuanzishwa, imekuwa na matokeo chanya lakini inakabiliwa uhaba wa fedha, hivyo kuna umuhimu wa kuiongezea fedha ili kutekeleza kwa ufanisi majukumu yake.

Pia alisema TARURA ina uhaba wa rasilimali watu akitoa mfano katika wilaya yake kuwa Meneja wa Wakala ana halmashauri tatu ambazo ni Manispaa ya Mtwara, Halmashauri ya Wilaya ya Mtwara na Halmashauri ya Mji Nanyamba, lakini kuna uhaba wa watumishi.

Aliliomba bunge kuchukua hatua za makusudi ili OR-TAMISEMI kupatiwa kibali kwa ajili ya kuajiri wahandisi ili wapelekwe katika wilaya na halmashauri kumaliza kero ya ubovu wa miundombinu ya barabara.

Mbunge wa Muleba Kusini (CCM), Oscar Ishengoma, alishauri serikali kuhakikisha TARURA inapatiwa vitendea kazi, yakiwamo magari ili kuwasaidia kufika na kukagua maeneo yenye uhitaji wa dharura na yafikiwe kwa kwa ajili ya matengenezo na kuwaongezea ufanisi zaidi kazini.

Mbunge wa Msalala (CCM), Iddi Khasim, alisema kutokana na mvua inayoendelea kunyesha kwa sasa, hali ya miundombinu imezidi kuwa mbovu, hivyo serikali inatakiwa kuiongezea fedha za dharura kusaidia kuirejesha katika hali yake pamoja na madaraja.

Naye Mbunge wa Nkasi Kaskazini (CHADEMA), Aida Khenani, alisema kuna muda fedha zinatengwa kwa ajili ya ukarabati wa miundombinu ya TARURA lakini nazo pia zinacheleweshwa hali inayosababisha maeneo mbalimbali kukosa mawasiliano. Ni vyema wapewe fedha kwa wakati ili watekeleze shughuli zao kwa ufanisi.

“Hili ni tatizo kubwa kwani kuna maeneo watu wanendelea kufa maji katika moja ya vivuko kutokana na kuwa kibovu kwa muda sasa, hivyo serikali ichukue hatua za dharura ili kuwahudumia wananchi,” alisema.

Mbunge wa Buhigwe (CCM), Kavejuru Felix, alisema licha ya kazi kubwa inayofanywa na TARURA, bado kuna mahitaji makubwa katika maeneo mbalimbali likiwamo jimbo lake, hususani wakati huu wa mvua iliyosababisha maafa makubwa katika miundombinu.

Alisema licha ya kuwa wamepokea fedha za dharura kwa ajili ya kurejesha hali ya miundombinu iliyoharibika, kuna maeneo mengine yenye uhitaji mkubwa ikiwa ni pamoja na eneo la Mto Mkoza kwenye barabara ya Mbanga - Lusaba ambako linahitajika daraja la kuunganisha mto huo.

“Pia tuna Mto Jujilo katika barabara ya Kibande - Butambuka ambako daraja pia lilikatika na kusombwa na maji kabisa, hivyo kufanya maeneo hayo kukosa mawasiliano. Naomba serikali kutoa msaada wa dharura kurejesha mawasiliano,” alisema.

Juzi, akiwasilisha makadirio ya Ofisi ya Rais- TAMISEMI lwa mwaka wa fedha 2024/25, Waziri Mohamed Mchengerwa alisema TARURA iliidhinishiwa Sh. bilioni 21 kwa ajili ya kazi za dharura na kwamba hadi Machi, mwaka huu, Sh. bilioni 50.43 zimepokelewa sawa na asilimia 240.14 kutokana na ongezeko la dharura lililosababishwa na mvua nyingi.

# Mgaga akwepa kifungo miaka 2 jela kukutwa hatia kuomba rushwa

**Na Halima Ikunji,** TABORA

MAHAKAMA ya Hakimu Mfawidhi Wilaya ya Nzega mkoani Tabora, imemhukumu Mtumishi wa Idara ya Afya ambaye ni mganga wa hospitali ya mji mdogo wa Nzega, Daudi Ashim Msokwa (29) kutumikia adhabu ya kifungo cha miaka miwili jela baada ya kukiri kosa la kuomba rushwa kutoka kwa mgonjwa aliyekuwa akitibiwa.

Awali, Mwendesha Mashitaka wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Wilaya ya Nzega, Mazengo Joseph, akishirikiana na Shabani Mntambo, wadai mbele ya Hakimu wa Mahakama ya Wilaya ya Nzega, Saturin Mushi, kuwa mshitakiwa April 16, mwaka huu katika hospitali ya mji mdogo wa Nzega aliomba rushwa ya Sh. 150,000 kwa Christina Aroiz (39), mkazi wa Nzega ambaye alikuwa amempeleka mgonjwa Gaudensia Eugene (25) aliyekuwa amelazwa na kufanyiwa upasuaji.

Joseph alidai mtuhumiwa aliomba kiasi hicho cha fedha kutoka kwa ndugu wa mgonjwa ili aweze kumruhusu kuondoka hospitalini hapo baada ya mtuhumiwa kumfanyia oparesheni.

Aidha, Mazengo alidai mahakamani hapo kuwa mtuhumiwa huyo alitenda kosa hilo kinyume na kifungu cha 15(1) (a), (2), (3)(a) cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa sura ya 329 marejeo ya 2002 inayozuia kutenda makosa kama hayo.

Mshitakiwa alikiri kutenda kosa hilo. Hata hivyo, Mwendesha Mashtaka Joseph alidai upande wa Jamhuri hawaoni sababu ya kupeleka mashahidi mahakamani kwa kuwa mshitakiwa amekiri mwenyewe.

Baada ya maelezo hayo Hakimu Mushi alisema: “Kwa kuwa mshitakiwa amekiri mwenyewe shitaka lake mbele ya mahakama inamtia hatiani mshitakiwa na kumpa adhabu ya miaka miwili jela au kulipa faini ya Sh. 500,000 ili iwe fundisho kwa wengine.

Mshitakiwa alilipa kiasi hicho cha fedha na kuwa huru.

HABARI KITAIFA

# Fursa kedekede ziara ya Samia Uturuki

**Na Christina Mwakangale**

RAIS Samia Suluhu Hassan, ameanza ziara yake leo, nchini Uturuki kwa mwaliko wa kiongozi mwenzake, Rais Recep Tayyip Erdogan.

Miongoni mwa majadiliano yenye vipaumbele ni kuimarisha uhusiano, elimu na fursa kibiashara kati ya nchi hizo, ambayo imekua kutoka dola milioni tisa za Kimarekani miaka sita iliyopita na kufikia milioni 22, mwaka jana.

Rais Samia, anatarajiwa kutia saini makubaliano kwenye maeneo sita kati ya 10 yaliyo katika mkakati, ikiwamo ufadhili wa masomo elimu ya juu, teknolojia, kuhifadhi nyaraka, sayansi pamoja na ubunifu.

Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, January Makamba, akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam, kabla ya ziara hiyo, alisema imeanza leo hadi Aprili 21 ni ya kipekee ikizingatiwa haijafanyika kwa miaka 14.

Makamba, alisema wakati Rais Samia akiwa nchini Uturuki, atapata fursa ya kuhudhuria kongamano la biashara na uwekezaji litakalofanyika mjini Istanbul, kuongeza wigo wa uwekezaji nchini na soko katika nchi hiyo.

"Kuna maeneo ambayo tunawekeana hati za makubaliano, mpaka hususan sita, tutaingia mikataba hasa elimu ya juu, kuhifadhi nyaraka, sayansi, teknolojia. Urari wa biashara kati ya nchi zetu, Uturuki wanauza zaidi kwetu kati ya dola 250,000.

"Miaka sita iliyopita biashara imepanda, mwaka jana, biashara ilifikia dola milioni 22 ukilinganisha na dola milioni tisa miaka sita iliyopita," alisema Makamba.

Alifafanua ukubwa wa uchumi wa nchi hiyo, ambao ni miongoni mwa nchi za barani Ulaya, ikiwa kati ya zilizo tajiri duniani, hivyo ziara hiyo ni muhimu na yenye tija kwa taifa.

"Tuna fursa kubwa ya kiteknolojia, kutoka kwao. Biashara kubwa kutoka Tanzania kwenda Uturuki ni mazao na vito. Tutaangalia maeneo mapya ya ushirikiano na dhifa, iliyoandaliwa na mwenyeji wake," aliongeza Makamba.

Kadhalika, biashara kubwa kutoka Tanzania, kwenda nchini Uturuki ni kahawa, nazi, tumbaku ghafi, minofu ya samaki, mchele na maharagwe, ambayo huuza bidhaa hizo kwa wastani wa dola milioni 15,99 kwa mwaka.


Pia kwenye uwekezaji wa kampuni za Uturuki uapande wa Tanzania bara, ni takribani dola milioni 414.23 katika sekta ya usafirishaji, uzalishaji, na utalii na ajira zinafikia 6,062.

**KUTUNUKIWA UDAKTARI**

Baraza la Chuo Kikuu cha Ankara, ambacho ni cha pili kwa ukubwa nchini Uturuki, limeamua kumtunuku Rais Samia Suluhu Hassan shahada ya heshima ya udaktari katika uchumi.

Uamuzi huo wa baraza ni kutambua uongozi wake wa kipekee, ambao umeleta mageuzi kijamii, kisiasa na kiuchumi Tanzania. Mageuzi hayo yameboresha ustawi wa Watanzania, kuimarisha sifa ya Tanzania duniani, kukuza uhusiano kibiashara, kiuchumi, kisiasa kati ya Tanzania na nchi zingine, ikiwamo Uturuki.

Hafla ya kukabidhiwa tuzo hiyo inafanyika leo katika Chuo Kikuu cha Ankara, ikiongozwa na Prof. Necdet Ünüvar ambaye Mkuu wa Chuo hicho. Hafla hiyo itahiduriwa na wanataaluma na wanafunzi wa chuo hicho na mabalozi wa nchi za Afrika, wanaowakilisha nchi zao Uturuki.




Katibu Tawala wa Wilaya ya Monduli, Anael Mbise (kushoto), akipokea moja ya madawati 130 kutoka kwa Meneja wa Benki ya NMB Kanda ya Kaskazini, Ladislaus Baraka, yaliyotolewa na Benki ya NMB kwa shule tatu za wilaya hiyo, wakati wa hafla iliyofanyika katika Shule ya Msingi Sokoine, wilayani humo jana. Wengine ni Mbunge wa Jimbo la Monduli, Fred Lowassa (wa pili kushoto) na Meneja wa Benki hiyo, Tawi la Monduli, Farida Kalufya. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mchungaji kizimbani madai ya kuchunga 'kondoo' bila kibali

**Na Grace Gurisha**

MCHUNGAJI wa Kanisa Joy's Testmony of Christ lililoko Kigamboni, Dar es Salaam, Godgiven Mushindikwa (52), raia wa Congo, amepandishwa kizimbani kwa mashtaka matano likiwamo la kufanya kazi za kichungaji bila kibali.

Mushindikwa alipandishwa kizimbani jana katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Gwantwa Mwankuga, na kusomewa mashtaka dhidi yake na mawakili wa serikali kutoka Idara ya Uhamiaji, Raphael Mpuya na Ezekiel Kibona.

Akisoma hati ya mashtaka, Kibona alidai kuwa mshtakiwa anadaiwa makosa hayo Aprili 4, 2024.

Kibona alidai kuwa katika shtaka la kwanza, Mchungaji Mushindikwa anadaiwa kuingia nchini kinyume cha sheria na Aprili 4, 2024 akiwa katika Ofisi za Uhamiaji zilizoko Kurasini, Dar es Salaam, alikutwa ameingia nchini bila kibali.

Ilidaiwa kuwa katika tarehe hiyo na eneo hilo hilo, mshtakiwa kinyume cha sheria alikutwa akiishi nchini bila kibali ndani ya mkoa wa Dar es Salaam.

Katika shtaka la tatu, Kibona alidai kuwa Aprili 4, 2024 mshtakiwa aliwasilisha nyaraka za uongo katika ofisi ya uhamiaji ili apate nyaraka za kusafiria.

Ilidaiwa kuwa Mchungaji Mushindikwa katika tarehe hiyo na eneo hilo, aliwasilisha cheti za kuzaliwa na kitambulisho cha Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) katika ofisi za Uhamiaji, vyote vikiwa na jina hilo na alivipata kwa njia ya uongo.

Wakili Kibona alidai kuwa katika shtaka la nne, mshtakiwa akiwa katika ofisi za Uhamiaji akidaiwa kuwadanganya maafisa wa idara hiyo kwa kuwasilisha nyaraka za uongo ili kupata hati ya kusafiria.

Pia alidai mshtakiwa katika tarehe hiyo akiwa raia wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, alikutwa akifanya kazi kama mchungaji katika Kanisa la Joy's Testmony Of Christ, Kigamboni bila kibali.

Baada ya kusomewa mashtaka hayo, alikana tuhuma hizo na aliachiwa kwa dhamana baada ya kutimiza masharti ya kuwa na wadhamini wawili waliotoka katika taasisi zinazofahamika.

Kesi hiyo iliahirishwa hadi Mei 9,2024 kwa ajili ya kusikilizwa hoja za awali.

## Shirika lakarabati chanzo maji kilichoathiriwa na maporomoko

**Na Mwandishi Wetu**

SHIRIKA WaterAid limekamilisha ukarabati wa miundombinu ya chanzo cha maji iliyoathiriwa na maporomoko ya tope, mawe na magogo katika kata ya Nangwa, Hanang' mkoani Manyara, kwa gharama ya Sh. milioni 127.4.

Desemba 3, mwaka jana, katika Wilaya ya Hanang' yalitokea maporomoko ya tope na mawe, magogo na maji kwa wingi kutoka mlima Hanang' kuelekea katika makazi ya watu.

Maafa ambayo hayakuwa mafuriko ya maji kama ilivyozoeleka na kusababisha madhara mbalimbali, ukiwamo uharibifu wa miundombinu ya maji katika kata nne ambazo ni Gendabi, Jorodom, Nangwa na Gitting.

Akizungumza katika hafla ya makabidhiano ya mradi huo jana wilayani Hanang', Mkurugenzi wa WaterAid Tanzania, Dk. Anna Mzinga, alisema baada ya maporomoko yale walilazimika kufika kusaidia kurejesha huduma ya maji.

Alisema WaterAid ikiwa ni moja ya wadau wakuu wa masuala ya maji na usafi waliitikia kwa ukubwa na kukarabati miundombinu ya chanzo cha maji iliyoathirika na kusababisha wakazi 26,900 kupata huduma tena.

"Kufuatia changamoto hii iliyoikuta wilaya ya Hanang mnamo mwishoni wa mwaka 2023, ilitupelekea sisi kuwa hapa siku ya leo kwasababu ili maisha ya mwanadamu yawe na utu na stara, tunaamini anapaswa kuwa na huduma za maji safi na salama pamoja na choo bora. "Kama shirika linalotekeleza miradi ya maji na usafi wa mazingira, tulisikumwa kukarabati chanzo hiki cha maji cha Nangwa ambacho kiliharibiwa vibaya sana na mvua kubwa," alisema Mzinga.

Alisema mbali na ukarabati wa chanzo cha maji, WaterAid ilitoa elimu ya usafi wa mazingira ya vyoo bora katika ngazi ya kaya kwa watoa huduma za afya, wenyeviti wa kata na vijiji ili jamii kuwa na utayari wa kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Serikali inastahili pongezi kupokea kilio cha kikokotoo

**KUNA** msemo kwamba ngoma ikivuma sana mwishowe hupasuka. Pia kuna msemo kwamba mzazi mzuri na bora ni yule amsikilizaye mwanawe kukusu matatizo yanayomkabili na hatimaye kuyapatia ufumbuzi.

Hivyo ndivyo inavyosadifu sasa kuhusu kilio cha miaka kadhaa kuhusu kikokotoo kipya cha mafao ya wastaafu baada ya Sheria ya Hifadhi ya Jamii kubadilishwa na kanuni mpya ya ukokotoaji mafao ilivyoanza kutumika tangu mwaka 2023.

Kanuni hiyo mpya inasema bila kujali wafanyakazi hapo ni wa umma au sekta binafsi, kikotoo cha mafao kitakuwa asilimia 33. Baada ya hapo, mnufaika atapata pensheni kidogo kidogo kwa muda wa miaka 12 na nusu na iwapo atafariki dunia, wategemezi wake watapewa kiasi hicho kwa miaka mitatu kisha kukoma.

Tangu kuanza kutumika kwa kanuni hiyo, kumekuwa na vilio vingi kutoka kwa watumishi kwamba kiasi wanacholipwa ni kidogo na kinakatisha tamaa. Vyama vya wafanyakazi kupitia shirikisho lao (TUCTA), pia vimekoleza mwangwi wa kilio kuhusu kikokotoo kabla ya kuwafikia wabunge ambao walisimama na kukizungumzia kwa uchungu katika Bunge la Bajeti linaloendelea mjini Dodoma.

Jambo kubwa lililowafumbua macho ni kuhusu uhalisia wa stahiki ya mtu anayestaafu uliotolewa na Mbunge wa Arusha Mjini (CCM), Mrisho Gambo. Akichangia makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Ofisi ya Bunge kwa mwaka wa fedha 2024/25, Gambo alisema kwa mtumishi aliyekuwa akipokea mshahara wa Sh. 800,000 kwa kikokotoo iliyokuwa mifuko ya wafanyakazi serikali za mitaa (LAPF) na watumishi wa umma (PSSF) alikuwa akipata malipo ya mkupuo Sh. 57,466,666 lakini kwa kikokotoo cha sasa anapata Sh. 28,675,862 tofauti ya Sh. milioni 29,190,804.

Mbali na mafao hayo, kila mwezi kustaafu alikuwa anapata Sh. 401,000 kwa kikokotoo cha zamani na cha sasa atapata 388,137. Hali hiyo inaonyesha wazi kwamba kuna uonevu mkubwa kwa wafanyakazi waliotumikia nchi kwa moyo wote kwa zaidi ya miaka 30. Baada ya kuibuka upya kwa mijadala mbalimbali ndani na nje ya Bunge kuhusu suala la kanuni mpya ya kikokotoo kipya cha wastaafu, hatimatye serikali imesema imepokea maoni yote yaliyotolewa na wadau pamoja na wabunge na kuahidi kulifanyia kazi.

Kauli hiyo ya serikali liyotolewa na Waziri Mkuu Kassim Majaliwa wakati wa kuhitimisha hoja ya makadirio ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Ofisi ya Bunge kwa mwaka 2024/25 Jumatatu wiki hii, ni ya kutia faraja na kurejesha matumaini ya wafanyakazi yaliyokuwa yamepotea. Kwa hatua hiyo, serikali imeonyesha ukomavu wake kuwa ni sikivu .

Bila kuuma maneno, Waziri Mkuu alisema serikali inatambua umuhimu wa kuboresha mafao kwa wastaafu na itaendelea kufanya tathimini kwa kuzingatia sheria za kazi. Pia alisema serikali itaendelea kutoa elimu ya hifadhi ya jamii ikiwamo mafao kwa watumishi kupitia njia mbalimbali kuhusu elimu ya mafao.

Kama alivyosema Waziri Mkuu Majaliwa, wafanyakazi na wadau wana matumaini makubwa kuwa serikali italifanyia kazi jambo hilo ambalo limeshasababisha maumivu kwa baadhi ya watumishi ili wanufaike na jasho walilovijisha kwa zaidi ya miaka 30 ya utumishi wao. Mafao bora kwa mstaafu ni kielelezo cha shukrani kwa utumishi wake uliotukuka ukiambatana na uaminifu kwa muda wote huo.

Kwa mantiki hiyo, serikali ikutane na wadau kupitia vyama vya wafanyakazi na waajiri ili kuweka sawa suala hilo ambalo halitoi picha nzuri kwa serikali. Jambo la muhimu ni kutambua kwamba mfanyakazi amekaa miaka 30 kwenye ajira, hivyo anatumaini kuwa kustaafu kwake kutampa Faraja na si majuto kama ilivyo kwa kikokotoo kipya.




Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com

## Muungwana Lazima Nilonge



Na Christina Mwakangale

# Giza hili kuelekea stendi ya Magufuli linatukwaza abiria kwa usalama wetu

**KITUO** cha Mabasi cha Magufuli kilichopo Mbezi, mkoani Dar es Salaam, kinatoa huduma za safari ziendazo mikoani na nchi jirani, huku kikitajwa kuwa na hadhi ya Kimataifa.

Hiyo inatokana na idadi ya huduma inazotoa kwa siku kwa ruti tofauti kwenda maeneo tofauti na Mabasi yanayokadiriwa kufikia 200 kwa siku.

Kwa sasa, unapoingia au kutoka kwenye kituo hicho kwa abiria wanaotembea kwa miguu inawalazimu kupita njia ya daraja la juu, ili kuwapa usalama watumiaji wa kituo hicho hususan abiria.

Uwapo wa giza kwenye daraja hilo hasa kwa watumiaji wa usiku imekuwa changamoto, kwa kuwa wanaolitumia iwe ni watu wenye ulemavu, wazee, watoto na makundi mengine ni hatari kwao.

Hata kwa usalama, pia inakuwa ni mdogo ikizingatiwa kwamba juu ya daraja kumezungukwa na wapiga debe ambao wao kazi yao ni kushawishi abiria watumie usafiri wao, lakini nani anajua kwamba wote kazi yao ni hiyo.

Kwenye msafara wa mamba na kenge wamo, huo ni msemo wa waswahili ambao naweza kuutumia hapa, kwa kuwa wapiga debe hao mbali na kukatazwa na mamlaka husika kufanya hivyo, kuna ushahidi unaotolewa mara kadhaa kwamba wapo na vibaka.

Giza hilo kwenye daraja hili isiwe fursa kwa watu wenye nia ovu na kutaka kuutumia mwanya huo kwa kuleta usumbufu kwa watumiaji hasa abiria.

Kama ambavyo inafahamika kwamba matumizi ya kituo hicho ni saa 24, kwa kuwa wapo wasafiri wanaotoka kanda mbalimbali ikiwamo ya Ziwa ambao huwasili kituoni zaidi ya saa sita usiku.

**Kwenye msafara wa mamba na kenge wamo, huo ni msemo wa waswahili ambao naweza kuutumia hapa, kwa kuwa wapiga debe hao mbali na kukatazwa na mamlaka husika kufanya hivyo, kuna ushahidi unaotolewa mara kadhaa kwamba wapo na vibaka.**

Mazingira rafiki ya kituo hiki yatakifanya kituo hicho kuwa salama kwa mtu yeyote hasa wageni na majira yeyote, mchana au usiku kwa kuwa, ni wakati wa mamlaka husika kuzingatia uwepo wa taa eneo hili.

Wakati mazingira ya watumiaji wa kituo hicho kuwalazimu abiria kupita juu ya daraja ni vyema eneo liwe na uhakika wa kulitumia daraja hilo, kwa kuweka taa na watu ambao hugeuza eneo hilo kijiwe wapigwe marufuku.

Kwa ilivyo sasa matumizi ya taa sio ya gharama, kwa kuwa kuna taa zilizoundwa kwa kutegemea chanzo cha jua mchana kutwa, kisha usiku taa zikawashwa bila gharama ya umeme utokanano na gharama za Tanesco.

Pia, daraja hilo lifanyiwe usafi kwa kuwa mara kadhaa usafi huwa duni, hujaa mchanga, taka za plastiki na makaratasi, uchafu ambao unashusha hadhi ya kituo hicho ambacho ni taswira ya mkoa na nchi kutokana na kupokea wageni wanaotoka nchi jirani kila uchao.

Kituo hicho kilizinduliwa Februari mwaka 2021 na Hayati John Magufuli, huku kikia na na uwezo wa kuhudumia mabasi 3,456 kwa siku, abiria 224,000 kwa siku na kuegesha magari madogo zaidi ya 280 na kuegeshwa mabasi 1000 wakati wa usiku.

Kadhalika, ofisi za mabenki, huduma za simu, hoteli, Ofisi za Uhamiaji, maduka pamoja na eneo la kupumzikia abiria na maliwato ni kati ya huduma muhimu zinazopatikana kituo hicho.

# Malecela awapigia chapuo vijana kuajiriwa kwa wingi

**Na Peter Mkwavila,**
CHAMWINO

WAZIRI Mkuu mstaafu, John Malecela amesema Tanzania hivi sasa inahitajika kutoa nafasi nyingi za uongozi kwa vijana ukinzingatia kuwa karibu asilimia 60 walio wengi ni kati ya wenye umri wa miaka 18 hadi 40

Alisema kuwa, kutokana na wingi huo wa vijana wanatakiwa kupatiwa nafasi za uongozi ili kuleta mabadiliko zaidi ya maendeleo ndani ya nchi.

Malecela alisema hayo alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari waliomtembelea kwenye shamba lake lililopo katika Kijiji cha Chamwino.

Alisema hivi sasa kwa zaidi ya asilimia 60 ya Watanzania wengi wao ni vijana kati ya umri wa miaka 18 hadi 49, nchi inahitaji kuongozwa na wao na wakipewa wataongoza vizuri.

"Tusiwe na mashaka nao hawa vijana wetu naamini wakipewa nafasi hizo wataongoza na kusimamia vema, kinachotakiwa ni kuwaamini na wanaweza kuongoza vizuri kama viongozi wengine waliopewa dhamana ya kuongoza na kusimamia ambao tunao kwenye nyanja mbalimbali za uongozi," alisema.

Aliwataka vijana kuchangamkia fursa ya kujiajiri kwenye sekta ya kilimo, badala ya kubaki kwenye manun'guniko ya kukosa ajira wakati ardhi ya kutosha kwenye halmashauri ipo.

Aidha, wasikate tamaa kwa ajili ya kukosa ajira serikalini kwa kuwa suala hilo lipo karibu ulimwenguni kote, badala ya kunung'unika wanatakiwa kuwa na mawazo ya kuibua miradi kwenye sekta ya kilimo.

Alisema bado serikali inaendelea kuwakumbuka na kuwajali kuwapatia ajira sekta mbalimbali, kinachohitajika kwa upande wao pia kubuni miradi itakayowafanya kuondokana na kufikiria kuajiriwa.

"Niwasihi vijana wangu kuwa ajira kubwa hapa nchini ipo kwenye sekta ya kilimo, niwaombe na kuwashauri wachangamkie fursa hiyo muhimu, badala ya kukaa na kunung'unika na kusubiri ajira za serikalini," alisisitiza.

Aidha, waendelea kumuunga mkono Rais Samia Suluhu Hassan kutokana na utendaji wake, ambao umeonyesha ndani ya uongozi wake umeleta mabadiliko makubwa na kuipaisha nchi kwenye nyanja mbalimbali ya miundombinu.



Waziri Mkuu mstaafu, John Malecela akiwaonyesha waandishi wa habari zao la mtama, walipotembelea shambani kwake katika kijiji cha Chamwino, wilaya ya Chamwino, mkoani Dodoma jana, kwa ajili ya kujifunza. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Musukuma: Makali kikokotoo yanazalisha watumishi wezi

**Na Vitus Audax,** DODOMA

MBUNGE wa Jimbo la Geita (CCM), Joseph Kasheku (Musukuma), ameitaka serikali kuchukua hatua za dharura kuhusu kanuni mpya ya kikokotoo cha mafao ya wastaafu ili kuepusha kuongezeka kwa watumishi wezi katika taasisi mbalimbali wanaotaka kujikwamua baada ya kustaafu.

Msukuma alitoa kauli hiyo jana bungeni wakati akichangia makadirio ya bajeti ya Wizara ya Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), kwa mwaka 2024/25.

Alisema ni wakati wa serikali kuliona suala hilo kama sehemu ya dharura kwa kuwa kila mkutano wa viongozi wakiwamo wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), limekuwa likiibuka na kushauri kurejesha kanuni ya awali ya asilimia 50.

"Kwa uelewa wangu mimi kama daktari wa akili, ninaona ni kama tunaenda kutengeneza taifa la watumishi wezi kwa sababu wanalalamika sana kuhusu suala la kikokotoo, kwa hali hii mstaafu anapewa kiasi kidogo cha fedha ambacho hakimtoshi hata kuanza maisha kwa hali hiyo lazima aibe kwasababu anajua hela zake hatopewa," alisema Musukuma.

"Juzi nilimsikia Katibu Mkuu wa CCM, Emamnuel Nchimbi akisema suala hilo haliwezi kuwa kilio cha kila siku na serikali inaendelea kuweka pamba masikioni (haisikii)," alinukuu.

Aidha, aliwataka mawaziri husika na serikali kukaa pamoja na kuona namna ya kurejesha kanuni ile ya awali ya asilimia 50 ili kuondoa vilio vya watumishi ambavyo alivitaja kudumu kwa muda mrefu.

"Kama kuna tatizo tuambieni maana hawa watumishi ni wetu, vinginevyo hakuna mtumishi atakuwa mwaminifu kwani unakuta amebakiza miaka mitatu ana watoto wamemaliza chuo kikuu na anatakiwa astaafu akajitegemee."

"Mtumishi huyo hana nyumba yupo nyumba ya serikali na anategemea kuondoka na asilimia 33 huyo lazima abebe mzigo aondoke nao," alisisitiza Msukuma.

Mbunge wa Jimbo la Chemba (CCM), Mohamed Monni, aliiomba Bunge kushughulikia suala hilo kama ilivyo dhamira ya Rais Samia Suluhu Hassan ili hali iwe salama.

"Kule nje inaonekana ni jambo ambalo hatuliongelei kabisa hivyo kwanini tuendelee kuishi na watu wenye manung'uniko makubwa wakati wanatusaidia kazi zetu," alisema.

Mbunge wa Iltilima (CCM), Njalu Silanga, alishauri Bunge lirudi mezani na kufanya utafiti wa kutosha kuhusu suala hilo ili kuona njia bora ya kuwasaidia wastaafu na kuendana na matarajio yao tofauti na sasa.


"Wazo la kuhamisha kikokotoo cha asilimia 50 kwa 50 kupeleka asilimia 67 kwa 33 lilikuwa ni jema, lakini hatukufanya utafiti vizuri ili kuendana na matarajio ya wastaafu kwani wamejiwekea kuwa wakistaafu atapata asilimia 50 ya Sh. milioni 100, lakini matokeo yake anaambiwa atapata asilimia 33 tayari hiyo ni shida," alisema.

Mwishoni mwa wiki iliyopita Katibu Mkuu wa CCM, Balozi Dk. Nchimbi akiwa mkoani Rukwa katika ziara yake ya mikoa sita aliahidi kufikisha hoja ya kikokotoo kwa Rais Samia kwaajili ya utatuzi, akisisitiza kuwa imekuwa kero kubwa kwa wastaafu.

Jana, Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa aliliambia Bunge kuwa serikali imepokea maoni ya wabunge na wadau mbalimbali kuhusu kikokotoo na kwamba litaendelea kufanyiwa kazi.

## KABWELA

Na Fadhili Mohammed






Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Alhaj Abubakar Kunenge (wa pili kushoto), akipokea msaada wa tani 20 za chakula na mitungi ya gesi na majiko yake 300 kutoka kwa Meneja Mkuu wa Kampuni ya Lake Energies, Nassoro Abubakari, wilayani Rufiji juzi, kwa ajili ya wananchi waliokumbwa na mafuriko. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# ATCL yaingia mkataba mashirika makubwa ndege kusafirisha watalii

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

BUNGE limeelezwa kuwa Shirika la Ndege Tanzania (ATCL), limeingia mikataba ya ushirikiano wa kibiashara na mashirika makubwa ya ndege ya kimataifa kwa ajili ya kusafirisha watalii kwenye maeneo ambayo mashirika hayo hayafiki.

Mashirika hayo ni pamoja na Qatar, Emirates, KLM, Air India, Ethiopia na Oman Air, ambayo huleta watalii Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere (JNIA) na Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Kilimanjaro (KIA).

Naibu Waziri wa Uchukuzi, David Kihenzile, alisema hayo bungeni jana alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Shaurimoyo (CCM), Ali Juma Mohamed.

Mbunge huyo alitaka kujua sababu gani zinafanya ATCL isitumie fursa ya kubeba watalii wanaotoka nchi mbalimbali duniani kuja nchini.

Akijibu swali hilo, alisema ATCL inatumia fursa iliyopo ya kusafirisha abiria wakiwamo watalii kwa kuanzisha vituo vilivyo karibu na vituo vya utalii nchini kama vile kituo cha Kilimanjaro na Arusha kwa watalii wanaotembelea Hifadhi ya Ngorongoro, Hifadhi ya Ziwa Manyara, Hifadhi ya Tarangire na Mlima Kilimanjaro.

Kituo cha Mwanza kuna hifadhi ya Serengeti, kituo cha Zanzibar kuna fukwe za bahari, hifadhi ya ghuba ya Johazi, msitu wa Pogwe pamoja na maeneo ya kihistoria.

Kituo cha Kigoma kuna hifadhi ya Gombe, kituo cha Mpanda kuna hifadhi ya Katavi na kituo cha Iringa kuna hifadhi za Mikumi, Ruaha na Kitulo

# Bil. 22/- zatengwa ujenzi bandari Bagamoyo

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imesema kwa mwaka 2024/25, kupitia Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA) imetenga Sh. bilioni 22 kwa ajili ya ujenzi wa bandari ya Bagamoyo.

Aidha, TPA imekamilisha ulipaji fidia kwa wananchi wanaopisha eneo la mradi lenye ukubwa wa hekta 887.

Naibu Waziri wa Uchukuzi, David Kihenzile, alisema hayo bungeni jana alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Subira Mgalu.

Mbunge huyo alihoji mpango wa ujenzi wa bandari ya Bagamoyo katika eneo la viwanda Bagamoyo umefikia hatua gani ya utekelezaji.

Akijibu swali hilo, Kihenzile alisema kwa sasa mradi huo uko katika hatua za mwisho za ukamilishaji wa uhuishaji wa taarifa ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina uliofanyika mwaka 2010.

"Kazi hii inatarajia kukamilika ndani ya mwaka huu wa fedha 2023/24 ili kuanza hatua za kupatikana kwa mkandarasi atakayejenga bandari hiyo. Aidha, katika mwaka wa fedha 2024/25, serikali kupitia TPA imetenga Sh. bilioni 22.00 kwa ajili ya kutekeleza mradi huo,"alisema.

Alibainisha kuwa ujenzi wa mradi huo utafanyika kwa awamu kulingana na matarajio ya ukuaji wa shehena na ongezeko la meli. Awamu ya kwanza itahusisha ujenzi wa magati matatu yenye urefu wa mita 1,000 na kina cha zaidi ya mita 15.5.

Pia alisema ujenzi wa bandari hiyo ni wa kimkakati kwa kuwa utachochea shughuli za viwanda na biashara katika eneo la ukanda maalum wa kiuchumi wa Bagamoyo.

# Mfanyakazi benki aliyempiga jirani nyundo akutwa na kesi ya kujibu

**Na Grace Gurisha**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kinondoni, Dar es Salaam imemkuta na kesi ya kujibu mfanyakazi wa benki, Ibrahim Masahi, anayetuhumiwa kumjeruhi na nyundo jirani yake Deogratus Minja kwa madai kuwa alikwenda kumshitaki serikali za mitaa kwamba anatiririsha maji machafu mbele ya nyumba yake.

Mahakama hiyo ilifikia uamuzi huo juzi, baada ya kusikiliza mashahidi wanne wa upande wa mashitaka katika kesi hiyo ya kujeruhi na kusababisha madhara katika mwili wa mlalamikaji inayomkabili Masahi.

Akitoa uamuzi huo, Hakimu Mkazi, Amos Rweikiza alisema baada ya kupitia ushahidi wote imeridhika kwamba mshitakiwa ana kesi ya kujibu kwa hiyo atatakiwa kujitetea.

"Mshitakiwa una haki zako hapa kuleta mashahidi, vielelezo na pia unaweza kutoa ushahidi wako chini ya kiapo au kukaa kimya," alisema Hakimu Rweikiza.

Wakili wa mshitakiwa alidai kuwa mteja wake atajitetea chini ya kiapo na pia hatokuwa na shahidi wala kielelezo chochote, kwa hiyo atajitetea mwenyewe. Kesi hiyo imeahirishwa hadi Aprili 24, mwaka huu, kwa ajili ya mshitakiwa kujitetea.

Masahi anatuhumiwa Januari 11, mwaka 2023 akiwa eneo la Mbezi Msakuzi, Wilaya ya Ubungo mkoani Dar es Salaam alimpiga Minja kwa nyundo na kumsababishia kupata madhara makubwa.

Katika ushahidi wake, Minja alidai kuwa tarehe hiyo saa 2.30 usiku alikuwa akipita nje ya geti la jirani yake Masahi, alimkuta kijana wa jirani huyo, baada ya kumuona alizungumza kwa kilugha kwa sauti kubwa ambaye yeye hakuielewa.

"Ghafla kijana alikuja mbele yangu akanizuia nisipite, mara geti likafunguliwa akatoka Masahi akanihoji kwamba mimi ni kama nani na kwenda kumshitaki serikali za mitaa, sikumjibu chochote kijana wake akanipiga ngumi." "Nilimgeukia jirani yangu ili amuonye kijana wake, lakini na yeye aliinua shati lake akatoa nyundo akanipiga nayo kichwani baada ya kupata maumivu makali nilianza kukimbia huku nikipiga kelele za kuomba msaada," alidai Minja.

Alidai kuwa alianguka chini ndipo Masahi akaanza tena kumshambulia na nyundo mgongoni, maumivu yalipomzidi aligeuka, akampiga na nyundo kwenye mkono wa kulia na kwenye bega. Jirani mmoja alifungua geti na kumsaidia kwa sababu alikuwa ana vuja damu nyingi na walimpeleka Hospitali ya Bochi kwa matibabu.

## HABARI KASKAZINI



# Mradi wa kuongeza ufaulu kwa wasichana waleta mafanikio

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

MRADI wa Back 2 School, unaolenga kuinua tija ya ufaulu kwa wasichana wa shule za sekondari zilizoko pembezoni umepata matokeo chanya wilayani Moshi, mkoani Kilimanjaro.

Mradi huo unawalenga wanafunzi wanaotembea umbali mrefu wa zaidi ya kilomita tano hadi 10 kwa siku kufuata masomo.

Akizungumza juzi katika hafla ya ugawaji wa baiskeli 60 kwa wanafunzi wa Shule ya Sekondari Mpirani iliyoko Kata ya Mabogini, Mkurugenzi wa Shirika la ABC IMPACT, Ayana Kimaro, alisema miongoni mwa changamoto wanayoipitia kwa sasa ni watoto wadogo kunyang'anywa baiskeli barabarani.

"Mradi wetu wa Back to School (Baiskeli kwenda Shule), asilimia 90 ya wanufaika ni wasichana. Mradi huu unatekelezwa katika mikoa minne ambayo ni Shinyanga, Dodoma, Arusha na Kilimanjaro.

"Kwa mwaka huu, tunagawa baiskeli 300 kwa awamu hii ya kwanza katika Mkoa wa Kilimanjaro, ikiwamo Kata ya Mabogini iliyoko Wilaya ya Moshi. Tunafahamu kwamba wasichana wanapitia changamoto ya umbali mrefu kufika shuleni na kutokana na changamoto hii wanakutana na matatizo kwa mfano na masuala ya unyanyasaji wa kijinsia, mimba za utotoni na ndoa za utotoni zinazokatisha lengo lao la elimu.

...Hivyo, tunaamini kwamba baiskeli hii tunayotoa itakwenda kumsaidia msichana huyu pamoja na kijana ili kutimiza ndoto yao ya elimu ili baadae waweze kusaidia familia zao pamoja na jamii kwa ujumla. Kwa mwaka jana pekee (2023) tuligawa baiskeli zaidi ya 1,000 na mwaka huu tunaamini tunakwenda kupambana ili tuweze kugawa baiskeli zaidi ya 1,000."

Kwa Wilaya ya Moshi, shule za sekondari zenye changamoto ya wanafunzi wa kike kukatisha ndoto zao kutokana na kutembea umbali mrefu na kutishiwa na mimba za utotoni, ni Mpirani, Oria, Mabogini, na TPC kwa Kilimanjaro.

Makamu Mkuu wa Shule Mpirani, Remmy Kaganga, akizungumzia mpango huo, alisema shule hiyo ina wanafunzi wa kike zaidi ya 300 wanaotokea umbali wa zaidi ya kilomita tano asubuhi na kurudi kilomita tano.

"Tunawashukuru ABC IMPACT kwa mradi wao wa Back to School, ambao umeleta tija kubwa sana katika shule yetu. Ukiangalia ni shule yenye wanafunzi 970 ikiwa na wavulana 500 na wasichana 470. Mradi huu wa baiskeli katika shule yetu umekuwapo kwa miaka minne na umewasaidia wanafunzi 416 mpaka kufikia leo.

"Ukichanganya na baiskeli 60 ambazo tunapata leo, tutakuwa na baiskeli 476. Kuna tija kubwa imeongezeka katika shule yetu hasa wasichana, ukiangalia tuna wanafunzi zaidi ya 300 wanatokea umbali wa zaidi ya kilomita tano asubuhi na wanatembea kwa miguu kwenda na kurudi.

Zaidi aliongeza: "Baiskeli hizi zitasawasaidia kuja shuleni kwa wakati na kurudi nyumbani kwa wakati. Tumeona mjongeo chanya katika matokeo, hasa kwa wasichana kwa kidato cha nne na kidato cha pili. Kwa sababu ukiangalia matokeo yanayotoka sasa hivi tunafanya tathimini kwa wanafunzi waliopata baiskeli wote wanafaulu hakuna wanaofeli."

Wakati huohuo, Mkuu wa Wilaya ya Moshi, Zephania Sumaye, ameonya kuhusu hujuma zinazofanywa na baadhi ya walimu, kufanya ulaghai kwa kutumia majina ya wanafunzi kujipatia baiskeli hizo isivyo halali na kwenda kufungua maduka yao na kuziuza kwa gharama kubwa.

Katika Mkoa wa Arusha, shirika hilo limejikita kuwasaidia wanafunzi wa kike wanaotembea umbali mrefu katika shule za Olorieni Sekondari, Olmot Sekondari, Olasiti Sekondari.




Mkuu wa Wilaya ya Simanjiro, mkoani Manyara, Fakii Lulandala (wa pili kushoto) akipokea zawadi ya saa ya ukutani yenye picha yake iliyotolewa na Chama Cha Mapinduzi (CCM), Wilaya hiyo, wakati wa hafla ya kumkaribisha baada ya kuripoti rasmi kikazi, juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Makonda kufanya kikao na mabalozi ili kuvutia watalii

**Na Beatrice Shayo,** ARUSHA

MKUU wa Mkoa wa Arusha, Paul Makonda, amesema anatarajia kufanya kikao kwa njia ya mtandao na mabalozi wa Tanzania waliopo nje ya nchi, ili kuangalia namna ya kutangaza fursa za utalii imkoani hapa, kuwavutia watalii wengi zaidi.

Alitoa kauli hiyo alipokutana na Balozi wa Tanzania nchini Ujerumani, Hassan Mwameta na Balozi wa Tanzania nchini Ubelgiji, Jestas Nyamanga, waliofika ofisini kwake kuzungumza naye kuhusu fursa zilizopo katika utalii.

"Mabalozi hawa ambao wanatuwakilisha katika taifa hili wanauzoefu, uelewa mpana kuhusiana na utalii wanaijua saiklojia ya mgeni atakapokuja katika nchi yetu na wanapata mrejesho wa mambo gani watalii wanayoyataka wanapokuja katika utalii," alisema.

Alisema atakapopata nafasi ya kufanya kikao na mabalozi hao watamweleza ni mambo gani ya kuwekewa mkazo ili kuhakikisha kuwa Tanzania inakuwa chachu ya chanzo ya kuwaleta watalii wengi.

Alisema mabalozi wamemuonyesha fursa zilizopo wao kama mkoa watachukua hatua kwa kuzikimbilia ili kuongeza watalii wengi mkoani Arusha.

Makonda alisema moja ya jambo ambalo linaingiza mapato kwa mkoa wa Arusha ni utalii, hivyo kila mmoja atatakiwa kupatiwa elimu ya utalii kwa upana ili kuongeza uchumi.

Alisema wataendelea kuboresha miundombinu ili kuhakikisha wageni wanapofika hawapati shida na suala la ulinzi litakuwa kipaumbele.

Makonda alisema wanataka kuwa na 'code' yaani mgeni akifika uwanja wa ndege kama mwenyeji umeenda kumpokea unakuwa na code yake atakapocheki inamuonyesha ni mtu sahihi anatambulika na serikali.

Mabalozi hao wamemueleza Makonda kuhusu fursa mbalimbali zinazopatikana kwenye nchi wanazoiwakilisha Tanzania na kuahidi kumpatia ushirikiano mkubwa katika kutangaza na kuvutia watalii ili wawekezaji kuja kutembelea mkoani Arusha na maeneo mengine yenye vivutio vya utalii.

# Dk. Jingu ahamasisha matumizi ya teknolojia ya habari

**Na Godfrey Mushi,** ARUSHA

KATIBU Mkuu wa Wizara ya Afya, Dk. John Jingu, amesema hataki kusikia watendaji wa wizara hiyo wanakuwa kikwazo cha matumizi ya teknolojia ya habari.

Badala yake ameagiza teknolojia hiyo iwe ni kichocheo cha kufanya ufuatiliaji na tathmini, ili kupata takwimu sahihi zitakazochangia kufanya maamuzi sahihi wakati wa kuandaa mipango ya bajeti kwenye sekta ya afya.

Alitoa agizo hilo jana Jijini Arusha, wakati akifungua kikao cha siku mbili, kilichowakutanisha wataalam wa TEHAMA na wale wa ufuatiliaji na tathmini zaidi ya 70.

Kikao hicho pamoja na mambo mengine, kinalenga kukuza ushirikiano baina ya wadau hao, uboreshaji wa programu na maendeleo ya jumla ya utoaji wa huduma kwenye kwenye sekta ya afya, ili kuwa na takwimu sahihi.

Kwa mujibu wa Dk. Jingu, ukuaji wa teknolojia unakwenda sambamba na mabadiliko ya mifumo ya TEHAMA, kwa kuiunganisha ili iweze kusomana, hali itakayochangia kuwa na tija na ufanisi wakati wa utekelezaji wa majukumu kwenye sekta afya na kupata matokeo chanya.

"Chochote tunachofanya katika dunia ya leo lazima tutumie TEHAMA, kwetu sekta ya afya hii ni ajenda muhimu sana kutokana na unyeti wa shughuli zetu, kosa moja linaweza kusababisha kukosekana kwa huduma, ulemavu na wakati mwingine kupoteza uhai wa mtu, hivyo kikao kazi hiki kitumike kutoka na maazimio yatakayokuwa na tija na ufanisi," alisema

Dk. Jingu ameagiza vilevile, mifumo ya TEHAMA itengenezwe katika wizara hiyo kulingana na mahitaji na kuzingatia teknolojia mpya na ya kisasa.

Mwakilishi wa Shirika la Afya Duniani (WHO) hapa nchini, Dk. Charles Moses, alisema dunia imekuwa na mabadiliko mengi kwa muda mfupi, hivyo kila mabadiliko yanapotokea husan ni kwenye teknolojia ya habari na mawasiliano, lazima vilevile na utendaji uendane na mabadiliko hayo.





# Wakazi Nyahanga walia kukithiri vibaka nyakati za usiku

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WAKAZI wa Kata ya Nyahanga, Halmashauri ya Manispaa ya Kahama mkoani Shinyanga wameiomba serikali kuingilia kati na kupambana na wezi wanaowavamia nyakati za usiku.

Wamesema wezi hao hutekeleza uhalifu wakati umeme unapokatika na kuwapora mali zao pamoja na kuwadhuru wananchi.

Walitoa malalamiko hayo wakati wa mkutano wa Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Mboni Mhita uliolenga kusikiliza na kutatua kero mbalimbali zinazowakabili wananchi.

Wakiwa katika kikao hicho walieleza kuwa wakati wa Sikukuu ya Paska waliibiwa na kuvunjiwa vibanda vyao vya bishara na hakuna mtu yeyote mpaka sasa aliyekamatwa kuhusika na matuko hayo.

Shadia Suleimani kutoka Mtaa wa Shunu alisema wamekuwa wakivamiwa nyakati za usiku katika makazi yao na vibanda vya biashara na kuibiwa mali walizonazo.

Hivyo, aliiomba serikali kuingilia kati na kutokomeza wizi huo kwani vibaka wengi wanatoka kwenye familia zinazowazunguka.

"Mkuu wetu suala hili tumeshariporti katika Ofisi za Serikali za Mitaa, Mtendaji wa Mtaa, Kata hadi kituo cha polisi lakini hakuna hatua zozote zilizochukuliwa, bado tunaendelea kuvunjia nyumba na vibanda vya biashara na kuibiwa, hivyo tunakuomba nawe utusaidie juu ya hili" alisema Suleiman.

Naye Shukuru Abdallah alisema katika bwawa la maji linalomilikiwa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Kahama (KUWASA) lililopo Kata ya Nyihongo kulipandwa miti na sasa kumekuwa kichaka cha kujifichia vibaka na kubaka watu wanaopita nyakati za usiku eneo hil.

Mkuu wa Polisi Manispaa ya Kahama, Mtaju Msiba alikili kuwepo kwa vibaka na wezi katika eneo hilo akisema Kata ya Nyihongo ndiyo inayoongoza kulinganisha na kata nyingine.

Hivyo, aliwataka wananchi hao kutoa taarifa kwa watu wanaowahisi kufanya vitendo hivyo kwani wengi wanatoka katika familia zinazowazunguka.

Baada ya kupokea hizo, Mboni alichukua hatua ya kuliagiza Jeshi la Polisi kufanya operesheni maalumu ya kutokomeza vitendo vya wizi na watakaohusika kujihusisha na vitendo hivyo hawakikishwe wanawachukulia hatua za kisheria ikiwemo kufikishwa mahakamani.

Pia, aliwataka wananchi kuacha tabia ya kununua vitu mitaani ambavyo hawafahamu vimetoka wapi akisema vingine vinapatikana kwa kumwaga damu za watu, Hospitali ya Manispaa ya Kahama kuna baadhi ya wagonjwa wanajeruhiwa na kuporwa simu na vitu vingine walivyonavyo nyakati za usiku.

# Waliopisha ujenzi mradi wa maji wajazwa manoti

**Marco Maduhu,** SHINYANGA

SERIKALI kupitia Wizara ya Maji imetoa Sh.milioni 444 kwa ajili ya kuwalipa fidia wananchi 97 kutoka vijiji sita wilayani Shinyanga, ambao walitoa maeneo yao kupisha mradi wa maji.

Ofisa Mazingira kutoka Wizara ya Maji, Moses Mgalla aliyasema hayo juzi wakati wa hafla ya wananchi hao 97 kusaini majendwali ya uthamini, ili waweze kulipwa fidia kupitia benki.

Alisema ulipwaji huo wa fidia umefuata taratibu zote za kisheria.

"Wananchi hao ni kutoka katika vijiji sita ambavyo ni Mwagala, Kolandoto, Ihapa, Kituli, Didia na Mwamakaranga ambao wamepisha maeneo yao kwa ajili ya mradi huu ambao utatekelezwa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Shinyanga (SHUWASA) na kufadhiliwa na Shirika la Maendeleo la Ufaransa (AFD) kwa ushirikiano na serikali" alisema.

Alisema ulipwaji huo umefikia hatua ya mwisho na wananchi walishirikishwa kuanzia hatua ya kwanza kwa kuainisha maeneo, kufanya uthamini na uhakiki pamoja na kutoa elimu, sasa wanakwenda kuwalipa pesa zao ili kupitisha utekelezaji wa mradi huo.

Alisema kuwa mradi huo unagharimu Euro milioni 76 sawa na Sh. bilioni 200 na unahusisha ujenzi wa mtandao wa majisafi, mitambo minne ya kuchakata tope kinyesi, ukarabati wa mtambo wa kutibu majisafi pamoja na kuijengea uwezo SHUWASA.

baadhi ya wananchi ambao wanalipwa fidia hizo akiwamo Kafula Ngaiwa kutoka Kijiji cha Ihapa, waliishukuru Serikali kwa kuwalipa fidia zao kwa wakati.

Aidha, walitoa wito kwa SHUWASA, kipindi cha utekelezaji wa mradi huo wakumbuke kuwapa ajira vijana wa maeneo yanayopitiwa na mradi.

Mwananchi mwingine, Paul Sitta, alisema wameridhika na fidia ambayo wanalipwa na kwamba wanabariki mradi huo kutekelezwa katika maeneo yao na kuahidi kuilinda miundombinu yake

Alisema: "Naishukuru serikali kwa kuweza kutukamilishia zoezi la kulipwa fidia ya ardhi walioichukua kwa ajili ya matumizi ya utekelezaji wa mradi huu na taratibu zote wamezifuata na tumeridhika na fidia ambayo tunalipwa".




Kaimu Kamanda wa Polisi mkoa wa Shinyanga, Kenedy Mgani akionyesha kwa waandishi wa habari mkoani humo jana, vitu mbalimbali vya wizi zikiwemo simu za mkononi, mafuta ya dizeli lita 320 na bangi kete 33, walivyovikamata katika msako uliofanyika kwa wiki tatu kuanzia Machi 28 hadi Aprili 16 mwaka huu. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Ahukumiwa kunyongwa hadi kufa kwa kumuua shangazi

**Na Neema Emmanuel,** SHINYANGA

MAHAKAMA Kuu Kanda ya Shinyanga imemuhukumu kunyongwa hadi kufa, Alex Masanja mkazi wa Mwigumbi wilayani Kishapu mkoani hapa kwa kosa la kumuua shangazi.

Ilielezwa mahakamani hapo kwamba Februari 16 mwaka jana mtuhumiwa alimpiga shangazi yake, Melisiana Malisa mkazi wa Kijiji cha Masagara wilayani Kishapu na kitu kizito kichwani baada ya kumzuia kutumia baiskeli yake.

Ilielezwa kuwa baada ya kutekeleza mauaji hayo mtuhumiwa aliiuza na kukimbilia kujificha wilayani Sikonge mkoani Tabora kwa mganga wa kienyeji.

Akisoma hukumu hiyo juzi lenye Shauri Namba 54 la Mwaka 2023, Jaji Seif Kulita alisema February 16 mwaka jana majira ya usiku Melisiana (marehemu) akiwa amelala alivamiwa na kupigwa na kitu kizito kichwani na mwili wake ulikutwa na majeraha kichwani pamoja na kuvuja damu.

Aidha, upande wa utetezi wa shauri hilo ukiongozwa na wakili Emmanuel Rugamila akizungumza baada ya hukumu kutolewa alisema wameipokea hukumu kama ilivyosomwa.


Alisema hukumu hiyo haimzuii mshitakiwa kutokukata rufaa, endapo itaonekana kuna haja ya kufanya hivyo japokuwa hukumu ya kunyongwa hadi kufa ni adhabu kubwa ambayo uwezi kuomba ufanye utetezi wa aina nyingine

"Tumepokea jinsi ambavyo Mahakama ilivyochambua na kutoa maamuzi, hakuna kesi ndogo kesi zote ni kubwa, lakini inategemea na ushahidi uliotolewa, mfano kesi hii ushahidi uliotolewa ulikuwa wa kimazingira lakini kwa sababu uliungwa mkono na mashahidi walioletwa na Jamhuri ndio maana Mahakama imeweza kufikia maamuzi haya " alisema Ruugamila.

Aidha, wakili wa serikali kutoka Ofisi ya Taifa ya Mashitaka mkoani hapa, Mboneke Ndimubeya alisema hukumu hiyo ni mafanikio makubwa kwao kwa sababu imeonyesha dhahili upande wa mashitaka wameweza kuthibitisha kosa la mauaji pasipo kuacha shaka yoyote.

Alisema mshitakiwa amepewa hukumu hiyo kutokana na ushahidi wa kimazingira ambao umejitosheleza moja kwa moja na unamgusa yeye ukiambatanisha na ungamo alilolifanya kwa hakimu.

ama
ALHAMISI APRILI 18, 2024
AFYA NA MAZINGIRA




Ukurasa 14

**Bima ya Afya kwenye simu, mgeni anayerahisisha huduma kidijitali**



Ukurasa 12

**MAISHA MAPYA...**

**Benki yawekeza 'CSR' Kanda Ziwa ikifuta vifo vya mama, mtoto wodini**



Ukurasa 13

EWURA walia kupotea maji, zao la mamlaka kutengua mwongozo wao

MAZINGIRA

# Wasimamizi mkaa wajipanga na staili ya uvunaji mkaa endelevu

## • Misitu ya miombo mtaji muhimu

**Na Christina Haule,** Morogoro

JUMUIYA ya Maendeleo ya nchi za Ulaya (EDF) kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha nchini, sasa zinajipanga kuwanufaika wananchi zaidi ya 58,000 kwa matumizi endelevu ya bidhaa za misitu.

Hiyo inagusa misitu aina ya miombo kutoka vijiji 13 vinavyotekeleza mradi wa Suluhisho Jumuishi la Misitu na Nishati hai Tanzania (IFBEST) katika wilaya nne za mkoa wa Tanga.

Meneja wa Mradi wa Miaka Mitatu, wenye thamani ya shilingi bilioni 5.4 ujulikanao kitaalamu 'Integrated Forest and Biomass Energy Solutions for Tanzania (IFBEST)' kutoka Shirika la Kuhifadhi Misitu Tanzania (TFCG) Simon Lugazo, anasema watahakikisha wanatoa elimu ya usimamizi bora wa misitu ya vijiji.

Hiyo inatajwa kama ilivyofanyika kwa vijiji 35 mkoani Morogoro, katika kuimarisha uhifadhi na kutokomeza shughuli za kibinadamu zinazosababisha uharibifu wa misitu. Lugazo anavitaja vijiji vya mkoani Tanga vitakavyonufaika na mradi huo; wilayani Handeni, ni; Gendagenda, Madebe, Kwamsisi, Mkalamo na Lusane, Mapanga, Nghobore, Mswaki, Sagasa/Kwa Mbogo.

Pia, anakitaja kijiji cha Mkonde wilayani Kilindi; wilayani Pangani kuna Mtango, Mseko na Kwakibuyu na vijiji kadhaa wilayani Mkinga.

Anasema, mradi huo utashughulikia masuala ya kuleta ufumbuzi endelevu wa uzalishaji wa mkaa, ambao anaueleza kitakwimu mkaa na kuni hutoa asilimia 93 ya nishati ya kupikia nchini.

"Mkaa huzalishwa kwa tani na kwa mwaka huzalishwa tani milioni 1.8, takriban asilimia 44.2 na hizo huwa ni changizo la Bilioni 2.1 katika idara ya misitu nchini," anasema Lugazo.

Aidha, Lugazo anasema uvunaji mkaa endelevu unaweza kufanyika na kunufaisha serikali na wananchi, kwakuwa asilimia 90 ya misitu nchini ni aina ya miombo, ambayo ina sifa ya kuchipua inapovunwa kitaalamu.

Hivyo, anaueleza mradi huo unakusudia kuandaa mipango ya ardhi na kuweka mipaka ya eneo la msitu wa kijiji kwa kuzingatia matumizi yaliyopo.

Lugazo anasema, mkakati walio nao utagawa msitu katika maeneo na vitalu; kama vile vyanzo vya maji, ufugaji nyuki, matambiko na eneo la uchimbaji madini jambo litakalosaidia kuondoa msongamano wa mambo na kuharibu utekelezaji.



Shughuli za ukataji kuni za mkaa zikiendelea mkoani Morogoro. **PICHA: CHRISTINA HAULE**

### MAFANIKIO MORO

Pia anautaja mradi huo ni matokeo ya mafanikio ya TFCG katika kuhifadhi misitu aina ya miombo uliofanyika mkoani Morogoro mwaka 2019/22 ambao hekta 133,579 zimehifadhiwa katika vijiji 35 vya mkoa.

Lugazo anaeleza kwamba, ukataji ovyo wa misitu umepungua kutoka asilimia 1.31 mwaka 2014 hadi kufikia asilimia 0.73 mwaka 2023.

Anasema, jamii kwa sasa vijiji hivyo 35 mkoani Morogoro zimenufaika kwa kupatiwa kiasi cha shilingi bilioni 2.09 kuanzia mwezi Disemba mwaka 2019 hadi Novemba 2022, zilizotokana na uvunaji endelevu wa mazao ya misitu kwenye vitalu vyao.

Inatajwa fedha hizo zimetumika kutekeleza miradi ya maendeleo kwenye vijiji vyao, ikiwamo ujenzi wa zahanati na vyumba vya madarasa, kukata bima za afya kwa ajili ya matibabu, kufungua biashara mbadala za kukuza uchumi wao.

### WAZITO WA MISITU

Mkurugenzi Mtendaji wa TFCG, Charles Meshack anasisitiza jamii kuona haja ya kuunga mkono usimamizi shirikishi wa misitu, huku akifafanua uzoefu uliopatikana.

Hapo anazitaja ni utekelezaji wa usimamizi shirikishi wa misitu ya jamii (CBFM) uliofanywa na mashirika hayo mawili kwenye mkoa wa Morogoro, inaonyesha mbinu hiyo ni dhana au rasilimali bora ya kupunguza upotevu wa miti nchini.

INAENDELEA UK.14

AFYA

MAISHA MAPYA...

# Benki yawekeza CSR Kanda ya Ziwa ikifuta vifo vya mama, mtoto wodini

**Na Mwandishi Wetu**

KITAIFA inaelezwa mafanikio yanayoendelea, imo kupungua vifo vya mama na mtoto. Ni matokeo ya kuimarika huduma za afya nchini, pia uwekezaji kiserikali na mchango wa wadau.

Hapo kuna sekta za umma na binafsi na Kanda ya Ziwa, sasa inatajwa kuwa sehemu ya mnufaika mkubwa wa vifaa tiba, inayotolewa na benki hiyo kuzisaidia hospitali na vituo vya afya.

Msingi wake azma ya serikali ni kuboresha ubora na kurahisisha upatikanaji wa matibabu na huduma nyingine mtambuka.

Kwa mujibu wa Mganga Mfawidhi wa Kituo cha Afya Buzuruga mkoani Mwanza, Dk. William Mtinginya, ufadhili umesaidia kupunguza kwa kiasi kikubwa vifo na maradhi, bali pia umesaidia kuongeza idadi ya akina mama na watoto wachanga wanaohudumiwa.

"Tumeweza kupunguza idadi ya vifo vinavyoweza kuzuilika vya wazazi na vichanga lakini pia wateja wa huduma ya uzazi wameongezeka na sasa wazazi wapya 20 wanahudumiwa hapa kwetu kila mwezi," Dk. Mtinginya anatamka wilayani Ilemela.

Takwimu zinaonyesha wastani theluthi moja ya vifo vyote vya watoto nchini vinatokana na watoto sababu zinazoweza kuzuilika, pia magonjwa yanayotibika pamoja na uhaba wa vifaa vya kuwahudumia.

Wataalamu wa afya wanafafanua kuwa vifo vingi vya hutokana na changamoto za afya za kinamama wanapokuwa wajawazito na mazingira duni ya kujifungulia

Hapo ndio wadau, benki ya NMB imeangaza shida hiyo na kuamua kuchangia, kuziba pengo la mapungufi katika afya kusaidia hali hiyo,

Kwa sasa, ufadhili wake umesaidia sana kulidhibiti kwa kiasi kikubwa tatizo hilo la kiafya katika Kanda ya Ziwa inayojumuisha mikoa minne, sasa viongozi, wanufaika Kanda ya Ziwa wanakiri imechangia kwa kiasi kikubwa kuboresha huduma za uzazi, mama na mtoto katika mikoa ya kanda hiyo; Mara, Kagera, Mwanza na Geita.

### KUTOKA NMB

Wawakilishi wa NMB makao makuu, wanasema vitanda vya kawaida na vya kujifungulia wazazi, magodoro na vifaa tiba vingine wanavyovitoa, vimekuwa ni uwekezaji wenye tija na afua muhimu katika kusaidia kuokoa maisha ya akina mama wajawazito na watoto.

Kwa mujibu wa sheria ya nchi, taasisi zote zina wajibu kurejesha faida kwa jamii, kupitia kinachoitwa kitaalamu kama 'corporate social responsibility.'

Ujumbe wa NMB ulikuwa katika ziara ya kutathimini shughuli za uwajibikaji wake kwa jamii katika mikoa mitatu ya kanda hiyo, ukifahamishwa uhalisia wa thamani hiyo inavyowaafikia wananchi; kuwaboreshea wana -afya mazingira ya kuwahudumia wazazi na watoto.

"Sambamba na dhamira yetu ya kurudisha fadhila kwa jamii, tunawekeza vya kutosha katika programu mbalimbali endelevu za kijamii kwa kila mwaka kutenga asilimia moja ya faida baada ya kodi katika shughuli za CSR," Meneja wa NMB Kanda ya Ziwa, Wogofya Mfalamagoha.

"Mwaka jana, bajeti hii ilifikia zaidi ya shilingi bilioni sita, pia kukidhi shughuli za uendelevu ambazo zilijumuisha upandaji miti kote nchini kwa ajili ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi," anasema Wogofya.

### TIMU YA MATABIBU

Mikoa iliyotembelewa ni Geita, Mara na Mwanza, huku Mganga Mfawidhi wa Kituo cha Afya Buzuruga mkoani Mwanza, Dk.William Mtinginya, akifafanua alivyonufaika na misaada hiyo:

"Tumeweza kupunguza idadi ya vifo vinavyoweza kuzuilika vya wazazi na vichanga, pia wateja wa huduma ya uzazi wameongezeka na sasa wazazi wapya 20 wanahudumiwa hapa kwetu kila mwezi."

Dk. Mtinginya anaiambia timu hiyo iliyomtembelea kituoni hapo wilayani Ilemela, kwamba: "Kabla ya ufadhili wa vifaa kutoka NMB tulikuwa tunawahudumia wajawazito 200 hadi 300 kwa mwezi. Lakini, sasa hivi wamefika 600, huku idadi ya wanaojifungulia majumbani nayo ikipungua sana."

Katika Kituo cha Afya Katoro mkoani Geita, Dk Rhoda Haule anaomba usaidizi zaidi kutoka taasisi nyingine za sekta binafsi, akisisitiza umuhimu na uhitaji wake katika kuyanusuru maisha ya wazazi na watoto wachanga.

Mganga huyo anataja moja ya faida za vitanda vipya ni kuondokana na changamoto ya kina mama kulala watatu hadi watano kwenye kitanda kimoja, wakisubiri kujifungua.

Anasema, pamoja na kuboreka huduma kwenye wodi za wazazi ambazo sasa zinawahudumia wajawazito kati ya 750 hadi 900 kila mwezi, bado kuna umuhimu wa kufanya maboresho zaidi.

"Jumla tuna vitanda 102, kwahiyo huduma zetu zitaimarika zaidi endapo tutapata wafadhili wengine," anaeleza

Benki hiyo, pia inapongezwa kwa msaada wa vitanda, mashuka na magodoro iliyopata zahanati ya Mwanangwa inayohudumia wakazi 20,000 wa Kata ya Mabuki na vijiji vya jirani wilayani Misungwi, Mwanza.

Dk. Consolata Simba, anasema huduma ya afya ya Mama nA Mtoto, ni suala mtambuka katika kuokoa maisha, kuimarisha ustawi wa jamii na kuchochea maendeleo ya taifa kwa ujumla.

Mganga huyo anasema, baadhi ya vifo vya mama na mtoto hutokana na umbali wa kufikia huduma stahiki, pamoja na kinamama kujifungua kienyeji majumbani.

Pia, anataja upungufu wa wahudumu wa afya wenye ujuzi wa kutosha, ukosefu wa vifaa tiba vya msingi, kutokuwepo kwa mfumo unaojitosheleza wa rufaa pamoja na huduma duni za dharura za uzazi na watoto wachanga.

Wataalamu wa afya za watoto wanasema vingi vya vifo hivi Hutokana na changamoto za afya za akina mama wanapokuwa wajawazito na mazingira duni ya kujifungulia na kuvilea vichango hali inayoonyesha unyeti wa mchango wa Benki ya NMB katika maendeleo ya sekta ya afya nchini.

Wilayani Serengeti, Mganga Mfawidhi Dk. Juma Rajabu Ali, anasema kujengwa wodi ya kisasa, ambayo ikikamilika mwezi ujao, itawezesha wajawazito wanne kujifungua kwa wakati mmoja, ikilinganishwa na wawili au watatu wanaojifungua kwa siku sasa.

Aidha, Dk. Juma anataja kuna manufaa ya kupunguzwa vifo vya watoto wachanga kwa sasa ni asilimia 12 hadi15, anafafanua: "Kupatikana ufadhili huu kwa wakati kusaidia kuukamilisha mradi huu wa ujenzi kumewagusa viongozi na wananchi kwa sababu ya umuhimu wake katika maisha ya wananchi wa hapa,"




Aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Missenyi mkoani Kagera, Kanali Wilson Akulo (watatu kulia) akipiga makofi, baada ya kupokea vitanda vya wagonjwa. **PICHA ZOTE: MPIGAPICHAWETU.**



Mganga Mfawidhi wa Zahanati ya Mwanangwa, wilayani Misungwi mkoa wa Mwanza, Consolata Simba, akionyesha baadhi ya vitanda, magodoro na mashuka walivyopokea.

> **"Pamoja na kuboreka huduma kwenye wodi za wazazi ambazo sasa zinawahudumia wajawazito kati ya 750 hadi 900 kila mwezi, bado kuna umuhimu wa kufanya maboresho zaidi.**

MAZINGIRA

# EWURA walia kupotea maji, zao la mamlaka kutengua mwongozo wao

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MAJI ni uhai. Hilo linajulikana tangu historia ya uhuru wa nchi. Hadi sasa, msimamizi mkuu, Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), inaongozwa ya mwaka 2019.

Kitaifa na kimataifa, kuna malengo ya maendeleo endelevu kufika mwaka 2030, Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025.

Mkurugenzi Mkuu wa EWURA, Dk. James Andilile, anasema uwezo wa miundombinu na uzalishaji maji umeimarika kwa asilimia 16.9, kutoka mita za ujazo milioni 744 hadi mita za ujazo milioni 870.

Andilile anasema, inaendana na kuongezeka uzalishaji maji kwa asilimia 1.8, kutoka mita za ujazo milioni 393 hadi mita milioni 400, huku wateja wa maji nao wakiongezeka kwa asilimia 11 kutoka, 1,385,485 hadi 1,532,362.

Hata hivyo, anataja baadhi ya viashiria vya utendaji wa mamlaka za maji vimezorota, kama vile kupotea maji, ufanisi wa ukusanyaji mapato na kuzingatia ubora wa majitaka.



Katibu Mkuu wa Maji Mhandisi Mwajuma Waziri, akikata utepe kuashiria uzinduzi wa Taarifa ya Utendaji kazi wa Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira kwa mwaka wa Fedha 2022/23 iliyoandaliwa na EWURA, jijini Dodoma. **PICHA: AGUSTA NJOJI**

### MIONGOZO YA EWURA

Andilile, anafafanua kuwa mamlaka za maji zimeshafanyiwa tathmini kwa kuzingatia Mwongozo wa Vigezo vya Utendaji wa EWURA kwa Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira wa Mwaka 2022.

Anafafanua kuwa, kilichofanyika ni kuangalia utendaji wa jumla katika kutoaji huduma za majisafi na usafi wa mazingira wa mamlaka za maji; vilevile utendaji unaozingatia kutekeleza malengo ya katika mipango yao.

Pia, anasema Mwongozo wa EWURA wa Kupunguza Upotevu wa Maji wa Mwaka 2021, umetumika kupima utendaji huo, ambao mamlaka za maji zinatakiwa kuhakikisha upotevu wa maji hauzidi asilimia 20 ya maji yanayozalishwa.

Kwa mujibu wa Mwongozo wa Kuchagua, Kufunga, Kupima na Kufanyia Matengenezo Dira za Maji kwa Mamlaka za Maji wa Mwaka 2021, mamlaka za maji zinatakiwa kuwa na sera, dira za maji na kanzidata, zitakazowasaidia kudhibiti upotevu wa maji.

### MAJI YANAYOPOTEA

Ripoti hiyo, inaonyesha upotevu wa maji dhidi ya kiwango cha maji kinachozalishwa umeongezeka kutoka asilimia 35.5 mwaka 2021/2,2 hadi kufikia asilimia 37.2 mwaka 2022/23.

Kiwango cha kupotea maji kinatajwa na ripoti kwamba, inachangiwa na utekelezaji dhaifu wa mikakati ya kupunguza kupotea maji.

Hapo mahsusi zinatajwa mamlaka maji 10 zenye kasoro kiasi ambazo ni: Kishapu, Maganzo, Busega, Nzega, Kashwasa, Mwanhuzi, Kasulu, Rujewa, Igunga na Kahama zilikuwa na upotevu wa maji chini ya asilimia 20.

Vilevile kuna zilizokuwapo katika hali mbaya na upungufu wa maji zaidi ya asilimia 50, ni mamlaka za maji 13, ambazo ni; Mahenge, Arusha, Mpanda, Vwawa-Mlowo, Makonde, Mpwapwa, Itumba-Isongole, Ifakara, Kiomboi, Rombo, HTM, Ushirombo na Mugango, pia Kiabakari.

Katika mwaka wa fedha 2022/23, mamlaka za maji 17 kati ya 85, ambazo ni DAWASA, Kahama, Moshi, Musoma, Shinyanga, Tanga, Bukoba, Bariadi, Makonde, Maswa, Biharamulo, Bunda, Igunga, Ngara, Nzega, Utete na Busega zilikuwa na mkakati wa kupunguza upotevu wa maji.

### MATOKEO YA UDHIBITI

Mkurugenzi - Andilile anasema matokeo yaliyopatikana kwenye sekta ya maji kutokana na udhibiti unaofanywa na EWURA kwa mamlaka za maji, ni pamoja na kupitia mipango iliyoandaliwa kwa kufuata mwongozo wa msimamizi huyo.

Hadi sasa, anazitaja mamlaka za maji zilizopunguza utegemezi serikalini, zikigharamia uendeshaji kwa kutumia mapato ya ndani na mikopo, kutekeleza miradi mikubwa, hata kufanikisha kuongezeka upatikanaji majisafi, pia kuhudumia majitaka.

"Mikataba hii umeimarisha utoaji wa huduma za maji na usafi wa mazingira," anasema

Pia, anasema mfumo imara wa kutatua migogoro kati ya watoa huduma na wateja na uwapo wa miongozo na kanuni zinazofanya mamlaka za maji zifanye kazi kwa uwazi, zinaongeza uwajibikaji kwa mteja.

"Kuwapo utaratibu bora na wenye gharama ndogo za maunganisho mapya, kwa wateja na kupunguza muda wa mteja kusubiri maunganisho, baada ya maombi yake na kufanya malipo," anasema Andilile.

Mkurugenzi huyo anasema, ni matokeo yanayotokana na ufuatiliaji wao, pia kuzijengea uwezo mamlaka za maji, ili kuhakikisha zinaandaa na kutekeleza mpango mkakati wa kupunguza maji yanayopotea nchini.

Hiyo inagusa katika maeneo ya sera za usimamizi wa dira za maji, mpango wa kufuatilia ubora wa majisafi na majitaka, pia mifumo ya utoaji taarifa za dharura kwa wadau na wananchi.

### KATIBU MKUU

Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji, Mhandisi Mwajuma Waziri, anasema atazichukulia hatua mamlaka ambazo utendaji wake hauridhishi, kwa kuwa na kiwango kikubwa cha upotevu huo na kusuasua kwenye ukusanyaji wa mapato.

> “ Kuwapo utaratibu bora na wenye gharama ndogo za maunganisho mapya, kwa wateja na kupunguza muda wa mteja kusubiri maunganisho, baada ya maombi yake na kufanya malipo.

Anasema: "Hii haikubaliki hata kidogo. Sote tunajua kiwango cha upotevu wa maji kinachokubalika ni chini ya asilimia 20. Ni lazima mamlaka za maji ziweke na kutekeleza mikakati ya kuhakikisha zinapunguza kiwango cha upotevu wa maji."

Anazitaka za maji nchini kuzingatia miongozo walinayo ya kudhibiti upotevu wa maji, kama vile 'Mwongozo wa Kupunguza Upotevu wa Maji wa Mwaka 2021' unaozitaka mamlaka za maji kuandaa mizani ya kupima viwango vya upotevu wa maji, kama zinavyoelekezwa na Mwongozo wa Jumuiya ya Kimataifa ya Wataalamu wa Maji (IWA).

Kuhusu ukusanyaji mapato, Mhandisi Mwajuma, anasema ripoti inaonyesha kushuka kwa jumla ya mapato yaliyokusanywa kutokana na huduma ya majisafi na majitaka na shughuli nyingine za Mamlaka kwa takribani asilimia mbili, kutoka shilingi bilioni 401.48 mwaka 2021/22 hadi shilingi bilioni 393.34, mwaka 2022/23.


"Inatarajiwa kuwa uzalishaji unapoongezeka basi na mapato yaongezeke. Mamlaka za maji ambazo zinajua zimezorota katika ukusanyaji wa mapato zijitafakari, sitakuwa tayari kufumbia macho watendaji wazembe,"anasema.

AFYA

# Bima ya Afya kwenye simu, mgeni anayerahisisha huduma kidijitali

**Na Mwandishi Wetu**

• Inatoboa kirahisi kusikofikika vijijini




DAR ES SALAAM Mwamko mdogo wa Watanzania kuhusu bima unaifanya Tanzania kukabiliwa na changamoto katika mpango wake wa kutoa huduma bora za afya kwa wote kutokana na kuwa na idadi ndogo ya Watanzania wenye bima ya afya.

Kwa mujibu wa takwimu za Wizara ya Afya (2022), ni takribani asilimia 15 tu ya Watanzania sawa na milioni 9.1 walikuwa na kadi za bima ya afya mwishoni mwa mwaka 2021.

Hiyo inaonyesha kupungua kwa kiasi kikubwa, ikilinganishwa na asilimia 32 iliyoripotiwa mwaka 2018, ambayo asilimia nane walikuwa na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), huku asilimia 21 ni wa chini ya Mfuko wa Afya wa Jamii ulioimarishwa (iCHF), asilimia tatu wakiwa kwenye mipango binafsi.

Katika kukuza ajenda ya maendeleo ya serikali, taasisi ya Vodacom Tanzania PLC, sasa imeungana na asasi ya Assemble Insurance, kurahisisha upatikanaji bima ya afya kwa njia ya dijitali kupitia bidhaa yake ya ubunifu ikiitwa AfyaPass.

Kinachofanyika, asasi Vodacom Tanzania inaendelea kutumia uzoefu wake kiteknolojia, pamoja na kuongezeka umiliki wa simu za mkononi, kuwawezesha watumiaji wake kupata bima ya afya kwa njia ya dijitali, bila kupitia taratibu ngumu za kujaza fomu lukuki, hata gharama.

Kwa mujibu wa wataalamu, kumekuwapo sababu zinazorudisha nyuma matumizi ya bima, hadi sasa, zikijumuisha umaskini mkubwa, uelewa mdogo kuhusu bima hizo, pia teknolojia duni.

Nyiginezo wataalmu wanazitaja ni kuwapo gharama kubwa zinazotolewa na ndani ya kampuni za bima na nyingi zimejaa mijini.

Akizungumza hivi karibuni jijini Dar es Salaam, Mkurugenzi wa M-Pesa kutoka Vodacom Tanzania, Epimack Mbeteni anasema, "Bidhaa yetu ya bima ya afya 'AfyaPass' inatoa huduma kwa wagonjwa wa kulazwa na ambao hawalazwi katika hospitali za serikali na binafsi nchini kote.

"AfyaPass inapatikana kupitia simu yako ya mkononi kupitia 'M-Pesa', na inalenga kurahisisha upatikanaji na kuongeza usawa katika matumizi ya bima kwa kila mtu.

"Ni bidhaa yenye gharama nafuu sana, inayopatikana kwa gharama ya shilingi 70,000 za Kitanzania kwa mtu mmoja kama ada ya mwaka," anasema.

Inaelezwa, kampuni chache zilizopo na kujielekeza katika biashara hizo zimejikita mijini, huku takwimu za Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA) ya mwaka 2022, inaonyesha Tanzania ilikuwa na kampuni 36 ya bima zinazohudumia watu milioni 62.

"Vodacom imerahisisha mchakato wa kukata bima. Unaweza kujiunga na VodaBima kwa kutumia simu yako ya mkononi ukiwa sehemu yoyote hapa nchini ikizingatiwa kuwa makampuni mengi ya bima yanapatikana katika maeneo ya mijini," anasema Juma Kweba, mkazi wa Singida.

Amani Nathaniel, ambaye ni mnufaika wa huduma ya bima AfyaPass, anasema ufahamu wake ulianza na tangazo aliloliona kwenye simu, kisha anasimulia hatua iliyofuata, akijitanguliza na sura ya tabasamu anatamka:

"Nilihamasika kujifunza zaidi kuhusu AfyaPass kwa sababu sisi kama vijana, wengi wetu tunaamini hatuhitaji bima ya afya kwa sababu hatupati maradhi mara kwa mara, kitu ambacho si kweli kabisa."

Huduma hiyo inatajwa kutoa vifurushi mbalimbali vya bei nafuu, kuanzia ada ya kila mwaka, inayotoa faida za tiba kwa wagonjwa wasiolazwa na wanaolazwa katika hospitali.

"Bima hii pia inatoa vifurushi vya familia au vikundi kuanzia watu wawili hadi sita. Mfano, watu wawili ni shilingi 105,000 na watu sita ni shilingi 385,000, ikiambatana na faida lukuki kutokana na aina ya kifurushi," anaeleza.

Pia, anafafanua ni ulingo unaompa uhuru wa kuchagua vifurushi zaidi, kama vile vinavyojumuisha uzazi, utambuzi wa maambukizi kwa picha (radiology), pia tiba maungo (physiotherapy).

Kanuni zake, ni pale mwanachama baada ya usajili, kitambulisho cha kidijitali cha bima hutolewa, ambacho ndio nambari yake ya uanachama itakayotumika kupata huduma za afya kwa watoa huduma walioorodheshwa nchini.

"Nilikuwa natumia gharama kubwa nilipokuwa sina bima ya afya, lakini AfyaPass imekuwa mkombozi wangu. Sasa naweza kupata huduma za afya wakati wowote na mahali popote nilipo," anasema Gift Kivuyo, mnufaika wa AfyaPass kutoka Dar es Salaam.

Kiujumla, bima ya afya inachangia asilimia 12 ya matumizi ya jumla ya afya nchini Tanzania, wakati malipo kwa fedha taslimu inayo asmilia 34; ufadhili wa serikali (24%); michango ya wafadhili (32%).

## Wasimamizi mkaa wajipanga na staili ya uvunaji mkaa endelevu

**INATOKA UK.11**

"Kuendeleza misitu kwenye ardhi ya kijiji kupitia CBFM huongeza ustahimilivu wa mabadiliko ya hali ya hewa na hivyo maeneo husika kuwa matokeo sahihi ya vipindi vya mvua na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi" Meshack anasema.

Hata hivyo, anasisitiza serikali kupitia wizara inayohusika inaendelea kusimamia marekebisho ya sheria na kanuni za misitu, ili kufanya USMJ kuendelea kutekelezeka na kuleta matokeo chanya.

Meshack anawasa wananchi kuwa wadau muhimu katika usimamizi na ulinzi wa maliasili zilizopo ambao hawana budi kuelimishwa namna ya kuzitumia kwa maendeleo endelevu.

Anasema, Shirika la Kuhifadhi Misitu Tanzania kwa ushirikiano wa Mtandao wa Jamii wa Kuhifadhi Misitu Tanzania (MJUMITA), wanatekeleza mradi huo kwa sasa wamejipanga kuweka dira ya kuhifadhi na kufuatilia usimamizi shirikishi ya misitu ya jamii ili kukomesha upoteza wa misitu ambao unaongezeka mwaka hadi mwaka.

"Kuendeleza misitu kwenye ardhi za vijiji kupitia USMJ huongeza ustahimilivu wa mabadiliko ya hali ya hewa, na hayo yatafanikiwa iwapo tu, marekebisho ya sera ya misitu kwa mujibu wa sheria na kanuni zitaendelea kuboreshwa " anasema Meshack.

Kwa mujibu wa Taarifa ya Tatu ya Mazingira nchini ya Mwaka 2019, takribani hekta 469,420 za misitu kwa mwaka hupotea kutokana na utegemezi mkubwa wa nishati ya kuni na mkaa kwa ajili ya kupikia.

Taarifa hiyo inasema katika kurejesha misitu hiyo inayokatwa kila mwaka nchini, wananchi wanalazimika kupanda na kutunza ukubwa wa hekta 185,000 ambayo ni sawa na miti 2,280,000 kwa mwaka kwa muda wa miaka 17 mfululizo.

Katika hotuba iliyosomwa mwaka 2022 katika Mkutano wa Wadau wa Misitu na Serikali uliofanyika jijini Dodoma, Mkurugenzi wa Misitu na Nyuki katika Wizara ya Maliasili na Utalii, Deusdedit Bwoyo anasema serikali ina mpango wa kusimamia halmashauri zote kutenga fedha za kuangalia misitu.

Anasema itakuwa katika bajeti za kila mwaka kwa ajli ya kuangalia misitu, sambamba na kutumika kwenye shughuli za usimamizi na uhifadhi wa misitu.

Bwoyo anafafanua kuwa kutengwa fedha kunapaswa kwenda sambamba na uwezo wa halmashauri, kwa sababu bado kuna wasiofahamu umuhimu wa misitu katika mazingira ya kawaida, wakiingia kukata kuni na wakifanya shughuli za uharibifu wa misitu zinazokatazwa.

Anasema Tanzania ina jumla ya misitu hekta mil 48.1, yakiwamo maeneo yanayoangukia katika ardhi za vijiji hekta milioni 22, kati yake ni chache zilizokidhi kuingia katika mpango wa usimamizi shirikishi.

Anasema, serikali kupitia wizara hiyo ipo katika mkakati wa kuhakikisha misitu mingi inahifadhiwa, kwa sababu iisipohifadhiwa kisheria, inakuwa hatarini kuharibiwa.

Hivyo, anasema tayari wameshatekeleza mkakati wa Sera ya Taifa ya Misitu, ambayo ndio dira ya kuendeleza misitu katika kipindi cha miaka 10 ijayo kuanzia mwaka 2021 hadi 203,1 ikiwa ni pamoja na kutengeneza mpango kazi wa usimamizi shirikishi wa misitu hasa katika vijiji wakilenga misitu mingi kuwa katika hifadhi za vijiji na kuhifadhiwa kisheria.

Anasema uhifadhi wa misitu ni wa pamoja tika Sera ya Misitu, sio wa Wizara ya Maliasili na Utalii pekee, pia wadau wa maendeleo kama, TFCG na MJUMITA kwa ajili ya kuendeleza misitu nchini.



# Bashe atishia kumtumbua Mrajisi Vyama vya Ushirika

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI wa Kilimo, Hussein Bashe, ameagiza Mrajisi wa Vyama vya Ushirika nchini, Dk. Benson Ndiege kumaliza suala la ubadhirifu kwenye vyama vinginevyo nafasi yake itakuwa matatani.

Alimpa agizo hilo jana jijini hapa alipokuwa akifungua mkutano mkuu wa 14 wa wadau wa kahawa nchini.

Bashe alisema suala la wizi katika vyama vya ushirika nchini linapaswa kukomeshwa mara moja kwani limekuwa moja ya sababu ya kuwanyonya wakulima.

"Kuna vyama vya ushirika viongozi wake wamechukua Sh.milioni 200 za wanunuzi wa kahawa lakini wamegoma kurejesha fedha hizo wala kutoa kahawa na deni hilo lote linabebwa na wakulima.

"Nakuagiza wizi huu na ujambazi unaofanywa katika vyama hivi unakwisha mara moja na mimi Ma DG wengi wa wizara hii ambao nimewaondoa kwenye nafasi zao ni kwasababu nilikua nawaambia kama hivi lakini hawachukui hatua"alisema Bashe

Alisema, viongozi wote ambao wamehusika kwenye wizi ndani ya vyama vya ushirika wanapswa kufikishwa mahakamani kwa kosa la wizi na siyo madai kama ilivyo sasa.

Aidha, alisema vyama vingi vya ushirika licha ya viongozi wake kuwa wezi lakini vimekuwa ni sehemu ya kunyonya wakulima kwa kuweka tozo nyingi.

Kadhalika, Bashe aliwata viongozi wa vyama vya ushirika kuandaa mahitaji ya wakulima na kuyawasilisha Bodi ya Kahawa ili yafanyiwe kazi. Mwenyekiti wa Bodi ya Kahawa, Prof. Aurelia Kamuzora, alisema malengo ni kuzalisha tani 300,000 za kahawa ifikapo mwaka 2025 kutoka tani 80 za hivi sasa.

Pia, aliwataka wakulima wa kahawa nchini kutumia mfumo rasmi wa uuzaji zao hilo na kujiepusha na walanguzi ambao wamekuwa wakiwadanganya kuuza kwa bei ya hasara.

Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo, Mariam Ditopile, alisema wataendelea kuisimamia serikali kutenga bajeti ya kutosha katika sekta ya kilimo.

Ditopile alisema ipo haja ya kuwekeza katika soko la ndani ili kuwa na uhakika kwa wakulima tofauti na ilivyo sasa ambapo kisi kinachouzwa nje kinaongezwa thamani na kurudi nchini kwa bei ya juu.



Baadhi ya Wabunge wakiwasili katika viwanja vya Bunge, jijini Dodoma jana, kwa ajili ya kuendelea na vikao vya bajeti vinavyoendelea. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Walimu, wanafunzi wapewa zawadi kwa ufaulu

**Na Thobias Mwanakatwe,** IRAMBA

WALIMU na wanafunzi wa shule za msingi wilayani hapa mkoani Singida wamepewa zawadi na Sh.milioni 14.5 kwa kufanya vizuri kwenye mitihani ya taifa ya darasa la nne na saba mwaka jana.

Motisha hiyo imetolewa na Mkuu wa Wilaya ya Iramba, Suleiman Mwenda, kwa walimu na wanafunzi 10 waliofaulu kwa kiwango cha juu kwenye mitihani hiyo.

Katika hafla hiyo, walimu waliofaulisha vizuri katika masomo yao, shule zilizoongeza ufaulu na zilizoongoza kwa kata zilipewa zawadi ya kompyuta.

Zawadi nyingine zilitolewa kwa shule bora sita zilizoongoza kiwilaya kwa ufaulu, kata, shule binafsi na shule iliyovunja rekodi kwa ufaulu.

Akizungumza na walimu hao, Mwenda, alisema kazi ya ualimu ni wito ambao unatakiwa kuitika kwa kufanya vizuri ili kuongeza ufaulu kwa wanafunzi wa shule yako.

"Najua uwezo wenu ndiyo maana pale ambapo panahitajika kuongeza nguvu tunachukua hatua na mimi kama kiongozi wenu naridhika na mabadiliko ambayo mnayaonyesha katika maendeleo ya elimu na kuongeza ufaulu," alisema.

Alisema alipoteuliwa kuwa Mkuu wa Wilaya Iramba alikuta kiwango cha ufaulu asilimia 58, lakini jitihada kubwa zimefanyika ndani ya miaka mitatu kiwango kimeongezeka na kufikia asilimia 71.9.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya hiyo, Michael Matomora, alisema haki ya mwalimu inatakiwa itolewe kwake lakini naye anapaswa kutekeleza wajibu wake.

Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Innocent Msengi, aliwataka maofisa elimu wa kata kuvua vyeo vyao na kushirikiana na walimu kuhakikisha Iramba inashika nafasi ya kwanza kimkoa.

Mwenyekiti wa Huduma za Jamii, Wilfred Kizanga, aliwataka walimu kishirikiana na kuondoka katika nafasi za mwisho kwani Iramba siyo mrithi wa nafasi

# Anwani za makazi milioni 12.3 zimesajiliwa, kuhifadhiwa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KATIBU Mkuu wa Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mohamed Khamis Abdulla amesema zaidi ya anwani za makazi milioni 12.3 nchini zimesajiliwa na taarifa zake zimehifadhiwa kwenye Mfumo wa Anwani za Makazi (NaPA).

Aliyasema hayo jana jijini hapa kwenye hafla ya kukabidhi vifaa na kuzindua majaribio ya kutoa huduma ya barua ya utambulisho wa mkazi kupitia mfumo wa kidijitali wa anwani za makazi.

Alisema Wizara kwa kushirikiana na TAMISEMI (Tanzania Bara) na TAMISEMIM na Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi (Zanzibar), imejipanga kuhakikisha uhakiki wa taarifa katika mikoa yote nchini unakamilika ifikapo Juni, 2025.

"Tumeendelea kusafisha na kuhuisha taarifa zilizokusanywa wakati wa operesheni ya anwani ya makazi kwa ajili ya kuwa na taarifa sahihi kila wakati ili kuleta tija, hadi sasa tumeshahuisha zaidi ya taarifa za anwani milioni 2.3 na kukusanywa taarifa mpya zaidi ya 500,000 kwenye halmashauri 28," alisema.

Alisema Wizara itahakikisha kuwa vishikwambi vinavyotolewa vinakuwa na intaneti, hivyo watendaji hawataingia gharama za ununuzi wa bando kwa muda wote wa kipindi cha majaribio ili kumhudumia mwananchi bila kikwazo chochote cha kimfumo.

Alisema majaribio hayo yatakuwa ya muda wa miezi mitatu na baada ya hapo Wizara itafanya tathmini na kuboresha kulingana na matokeo ya tathmini husika.

# Dk. Biteko aishukia TGDC kushindwa kuchoronga visima

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

NAIBU Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko ameinyooshea kidole Kampuni ya Uendelezaji Jotoardhi Tanzania (TGDC) kutokana kusuasua kuanza kuchoronga visima vya jotoardhi katika eneo la Ngozi mkoani Mbeya.

Akifungua Maonesho ya Wiki ya Nishati bungeni juzi, Dk. Biteko alisema TGDC ni miongoni mwa kampuni tanzu za Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) ambapo Aprili Mosi, 2024 ilitoa ahadi ya kuanza kazi hiyo lakini hadi sasa hawajaanza.

"TGDC nimewawashia taa ya tahadhari, nilipokwenda Mbeya waliniambia wanaanza kuchoronga Aprili mosi mwaka huu kwa ajili ya kupata geothermal ili kupata umeme, naomba Katibu Mkuu tupia jicho kasi iongezeke,"alisema.

Alisema kwa sasa kuna umeme wa kutosha, lakini tatizo la kukatika linatokana na uchakavu wa miundombinu na kwamba serikali imejipanga kuifanya TANESCO kuwa na jina zuri kwa jamii ili iondokane na mtazamo hasi kwamba kila umeme giza likitokea au umeme ukikatika tatizo ni wao.

Kadhalika, alipongeza utendaji wa TANESCO kwamba wanafanya kazi nzuri usiku na mchana kuhakikisha wananchi wanapata huduma ya umeme.

Dk. Biteko alisema kutokana na kuwapo na umeme wa kutosha hata kituo cha umeme cha Kinyerezi megawati 150 hakijawashwa na kueleza kuwa hali hiyo imetokana na kuendelea kuwasha mashine za mradi wa umeme wa Bwawa la Mwalimu Nyerere.

Alisema mkakati mwingine wa Serikali ni kuhakikisha kwamba Tanzania inaunganishwa na nchi jirani ikiwamo Zambia, Uganda na Kenya.

Naibu Spika wa Bunge, Mussa Zungu alipongeza juhudi za serikali za kutatua tatizo la umeme na kwamba kwasasa makundi ya mitandao ya kijamii ya kukatika kwa umeme kwasasa hayazungumzii tatizo hilo.





# Prof. Mkenda awatwisha mzigo makatibu tawala upatikanaji wa chakula shuleni

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MAKATIBU tawala nchini wameagizwa kushirikiana na wakurugenzi, madiwani, wazazi na wadau wengine wa elimu kuhakikisha wanafunzi wote wa shule za awali, msingi na sekondari wanapata chakula cha mchana shuleni kwa lengo la kuongeza ufaulu.

Waziri wa Elimu, Sayansi na Mafunzo ya Ufundi, Prof. Adolf Mkenda alitoa agizo hilo juzi kupitia hotuba yake ya ufunguzi wa mkutano mkuu wa mwaka wa Chama cha Maofisa Elimu wa Mikoa na Halmashauri nchini (REDEOA) ambao unaendelea mkoani hapa.

Hotuba hiyo ilisomwa na Mdhibiti Ubora wa Elimu wa Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Edo Masonda ambapo alisema agizo hilo ni utekelezaji wa sera ya elimu na kwamba kila kiongozi anatakiwa kusimamia kwenye eneo lake na kwamba tathimini itakuwa inafanyika.

Aidha, aliagiza maofisa elimu kushirikiana na wadau wengine kuhakikisha wanafunzi wote wa darasa la kwanza na la pili wanamudu stadi za kusoma, kuandika na kuhesabu (KKK) ifikapo mwisho wa mwaka.

Vilevile aliagiza maofisa elimu wa mikoa na halmashauri kusimamia na kuhakikisha miradi yote ya elimu inakamilika kwa wakati na kwa viwango vilivyoainishwa.

"Lakini pia kila ofisa elimu wa mkoa na halmashauri ahakikishe wanafunzi wa darasa la tatu na kidato cha kwanza wanamudu stadi za Lugha ya Kiingereza ifikapo mwisho wa mwaka," alisema Mkenda.

Hata hivyo, aliwataka viongozi wote wa elimu kuwahudumia walimu kwa kufuata misingi iliyowekwa na kuwasaidia kutatua kero zinazowakabili ili wafanye kazi kwa uhuru.

Mwenyekiti wa REDEOA, Juma Kaponda alisema wasimamizi wa elimu nchini wana kazi ya kuhakikisha malengo mbalimbali ya serikali yanatimia, ikiwemo kuboresha sekta ya elimu ambayo ni miongoni mwa mikakati wanayojadiliana kwenye mkutano huo.

Alisema mwaka 2024 ni mwaka muhimu kwa viongozi hao na kwamba kwenye mkutano huo wanajadili namna ya kutekeleza Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 ambayo utekelezaji wake unaanza mwaka huu.

Alisema serikali imekuwa ikiandaa mipango mbalimbali na watekelezaji wake unasimamiwa moja kwa moja na maofisa elimu pamoja na walimu kwa ngazi mbalimbali.

"Mwaka huu ni mwaka wa historia kwetu kwa sababu ndiyo mwaka ambao tunaanza utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014, kwa hiyo sisi maofisa elimu tuna kazi kubwa ya kufanya kuhakikisha utekelezaji unaendana na malengo ya serikali," alisema Kaponda.

Katibu wa REDEOA, Sostenes Mbwilo aliiomba serikali kuharakisha uboreshaji wa muundo wa wadhibiti ubora wa elimu katika halmashauri ili kurahisisha uendeshaji wa shughuli za sekta hiyo.

Vilevile, aliomba serikali kuboresha mfumo wa ukusanyaji wa maduhuri kwenye vyuo ili kurahisisha utoaji wa huduma kwa wanafunzi kwenye taasisi hizo.

Makamu Mwenyekiti wa REDEOA, Charles Mwakalila aliomba serikali kuweka utaratibu wa matumizi ya magari ya idara ya elimu kwenye halmashauri kwa maelezo kuwa baadhi ya viongozi wamekuwa wakibadili matumizi.



Wakazi wa Kata ya Itamboleo, Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali, mkoani Mbeya, wakivua samaki kwa kutumia ndoano kwenye mfereji wa skimu ya umwagiliaji iliyopo katika kata hiyo, juzi. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Silaa: Watumishi Wizara ya Ardhi kuweni na hofu ya Mungu

**Na Mwandishi Wetu,** MBEYA

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Jerry Silaa amewataka watumishi wa ardhi nchini kuwa waadilifu na hofu ya Mungu kwa kutenda haki wakati wanaposuluhisha migogoro.

Aliyasema hayo jana wakati akifungua kliniki ya ardhi Mkoa wa Mbeya.

Pamoja na mambo mengine aliwakumbusha watumishi wa ardhi kutenda haki kwa wananchi kwani kwa kushindwa kutatua jambo ambalo lipo ndani ya uwezo wao ni kumkosea Mungu.

Aidha, Silaa alisisitiza kufanya kazi kwa kumsaidia Rais Dk. Samia Suluhu Hassan lakini pia kufanya kazi kwa ajili ya wananchi katika upande wa ardhi ili kupunguza kero na migogoro isiyokuwa na ulazima katika jamii.

Pia, aliwaelekeza watumishi wa ardhi kuhakikisha maeneo yote nchini yanapangwa na kupimwa.

"Nimeelekeza juzi na Septemba mwaka jana nilielekeza na nimemuomba Waziri wa TAMISEMI atawaletea barua kwamba watumishi wa ardhi wakae ofisini,siku ya Jumatatu na Ijumaa tu," alisema Silaa.

Aliongeza kuwa: "Siku zingine zote waende site (eneo la kazi) wakapange kila mtu akafanye kazi kwenye eneo lake, wa mipango miji wakapange, wakupima wakapime, maofisa ardhi wakamilikishe, wathaminishaji wakatengeneze rate (thamani) za ardhi," alisema.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera alimpongeza Silaa kwa kuitumikia vyema sekta ya ardhi kwa kutatua migogoro mbalimbali nchini ikiwa ni moja ya jitihada za kumsaidia Rais Samia Suluhu Hassan kwa vitendo.

# Baba mbaroni tuhuma kumbaka mtoto wake

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

JESHI la Polisi mkoani Njombe linamshikilia mkazi wa Mtaa wa Kitisi Halmashauri ya Mji wa Makambako mkoani Njombe, Barnabas Ndelwa (32) kwa tuhuma za kumbaka mtoto wake (13).

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Njombe, Mahamoud Banga aliiambia Nipashe kuwa tukio hilo lilipotiwa Aprili 14 katika wilaya ya kipolisi Makambako.

Banga alisema taarifa hizo walizipata kutoka kwa mtoto alipofika na baba yake kituoni hapo kwa ajili ya huduma nyingine.

"Tukio hili limekuwa likitendwa na baba mzazi tangu mwaka 2022 na binti alipofika kituo cha polisi kwa ajili ya kupata huduma ya PF3 ndipo alipowaeleza maofisa wa dawati la polisi kwamba licha ya tukio ambalo ameletwa na mzazi wake kwa masuala ya kijinsia lakini bado na baba yake mzazi alikuwa anamuingilia," alisema Kamanda Banga.

## Mama Maria Nyerere apewa tuzo ya heshima

**Na Mary Geofrey**

SHULE ya Sekondari ya Wavulana Pugu, imemtunukia tuzo ya heshima, mjane wa Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, Mama Maria Nyerere.

Dhumuni la tuzo hiyo ni kuendelea kutambua mchango wa Mwalimu Nyerere katika ukombozi wa Tanzania, Afrika na sekta ya elimu nchini.

Mwalimu Mkuu wa shule hiyo, Boniface Orenda, alikabidhi tuzo hiyo mwishoni mwa wiki nyumbani kwa mjane huyo Msasani mkoani Dar es Salaam.

Alisema Hayati Mwalimu Nyerere ambaye alifundisha shule hiyo, hakuwa tu na mchango mkubwa kwa Tanzania pekee bali dunia kwa ujumla, ndiyo sababu ya kuona umuhimu wa kuendelea kutoa tuzo ya kutambua mchango wake.

"Kwa kutambua mchango huu wa Hayati Mwalimu Nyerere, tumeona kuna umuhimu wa kuja kumuona mama yetu, kumjulia hali lakini na kutoa tuzo na zawadi mbalimbali kwa kutambua mchango wake kama Bibi wa Taifa letu," alisema Orenda.

Alisema shule hiyo imekuwa na mafanikio makubwa kutokana na historia yake ya kuwahi kuwa na mwalimu ambaye alikuwa mkombozi wa Afrika.

Alisema: "Tunamwomba Mungu akujalie umri mrefu na afya njema mama yetu Maria Nyerere ili tuendelee kuvuna baraka kutoka kwako na mawazo yenye kujenga taaluma yetu".

Shule ya Sekondari Pugu zamani ilijulikana kama St. Francis ambayo ipo eneo la Pugu, Gongo la Mboto, jijini Dar es Salaam. Alisema: "Unajua shule hii ni kongwe sana na ilianza mwaka 1948 na sasa ina miaka 75, hivyo lazima tufanye kazi kwa bidii sana katika kuhakikisha historia ya kutoa viongozi wakubwa kwenye shule yetu inaendelea na huu ndiyo mkakati wetu tunaomba Mungu atusaidie".





# Polisi yawashikilia watu 21 wakituhumiwa kwa uhalifu

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

JESHI la Polisi mkoani Mjini Magharibi Unguja limefanikiwa kuwakamata watuhumiwa 21 wanaojihusisha na matukio ya wizi, uporaji na unyang'anyi wa kutumia nguvu na silaha za jadi.

Kamanda wa Polisi Mkoa huo, Richard Tadei Mchovu aliyasema hayo jana wakati akizungumza na vyombo vya habari, ofisini kwake Mwembe Madema mjini Unguja.

Alisema watuhumiwa hao wamekamatwa wakati wa operesheni maalumu ambayo imewafikia wahalifu na sehemu zao wanazoficha mali na vitu wanavyoiba katika maeneo mbali mbali.

Aliwataja watuhumiwa hao ni Bilali Makame Faki, (20), Masoud Juma Kombo, Daudi Mussa Mlekwa (20), Said Juma Feruzi (20).

Wengine ni Salum Abrahman Ali (21), Abdilah Rashid Ali (18), Yussuf Hamad Ali (17) Masoud Ahmed Khatib (17) Ali Hamad Ali, (25) na Omar Salum Bakari (18) Ali Mkadam Khamis (28).

Wengine ni Faki Juma Omar (19), Hussein Mohammed Said (21) Ali Omar Ali (38), Abdul aziz Juma Khamis (18),Ibrahim Salum Khamis (27) na Mohammed Ali Omar (32).

Aidha alisema katika operesheni hiyo Jeshi la Polisi limefanikiwa kukamata vielelezo mbalimbali ikiwemo pikipiki moja, mapanga nane, visu na simu tatu.

Kamanda Mchovu aliwataka wananchi kutoa ushirikiano kwa jeshi hilo ili kuhakikisha vitendo vya udhalilishaji na matukio mengine ya kihalifu vinakoma.

Alisema yoyote atakaejaribu kujihusisha na vitendo vya uvunjifu wa amani, vitendo viovu pamoja na kujipatia kipato kwa njia isiyo halali atachukuliwa hatua.

# Dk. Mwinyi: Mapambano ya rushwa yanachochea maendeleo

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, DK. Hussein Ali Mwinyi amesema, mapambano dhidi ya rushwa, kuwepo kwa uwazi katika matumizi ya rasilimali za umma na kuhimiza uwajibikaji katika utekelezaji wa mipango ya maendeleo, ni mambo ya msingi na yenye mchango muhimu katika kuchochea kasi ya maendeleo.

Dk. Mwinyi alisema hayo jana visiwani Zanzibar wakati akifungua kongamano la kamati za usimamizi wa fedha za umma kwa nchi wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADCOPAC) lililofanyika visiwani hapa.

Alisema ni dhahiri kuwa nchi zitaweza kupiga hatua kubwa za maendeleo kwa haraka kwa kuzingatia kuwepo kwa rasilimali nyingi ambazo ni vyanzo vikuu vya kukuza uchumi, ikiwa vitasimamiwa vyema na kutumika kwa misingi ya kisheria, uwazi na uwajibikaji.

"Bila shaka taasisi zetu za utawala bora zikiwemo Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Mamlaka za kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi na mabunge yetu yana mchango mkubwa katika kuyafikia matarajio hayo ya mataifa yetu," alisema Dk. Mwinyi.

Alisema kuwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar zinafanya jitihada katika kukabiliana na vitendo vya rushwa na kuhimiza uwazi na uwajibikaji ili kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma kwa umma.

Aidha, alisema mbali ya kuzijengea uwezo taasisi hizo kwa mafunzo ili kuzipatia weledi, pia inazipatia vifaa vya kufanyia kazi pamoja na kuzijengea miundombinu bora ili ziweze kufanya kazi kwa ufanisi zaidi.

Aliongeza kuwa hatua nyingine ni kujadiliwa kwa uwazi kwa ripoti ya CAG katika Baraza la Wawakilishi, uimarishaji wa Mamlaka ya Kupambana na Rushwa na Uhujumu wa Uchumi (ZAECA) na Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashitaka (DPP) kulikosaidia kufikiwa kwa malengo ya uimarishaji utawala bora nchini.

Aidha, alipongeza uamuzi wa jumuiya hiyo kufanya kongamano hilo Zanzibar na kueleza kuwa mapambano dhidi ya vitendo vya rushwa, kuwepo kwa uwazi katika matumizi ya rasilimali za umma na kuhimiza uwajibikaji katika utekelezaji wa mipango yetu ya maendeleo katika kukuza uchumi wa nchi zetu.

Hata hivyo, alipongeza uamuzi wa jumuiya hiyo kufanya kongamano hilo Zanzibar ambalo litawawezesha wajumbe kutoka nchi wanachama kupiga hatua za maendeleo kwa haraka kwa kuzingatia uwepo wa rasilimali nyingi zinazoweza kuwa vyanzo vikuu vya kukuza uchumi.

Pia, alitoa wito kwa nchi wanachama wa SADC kuziimarisha taasisi za ukaguzi na ufuatiliaji rasilimali za umma kwa kuzipatia wataalamu wa fani mbali mbali ili ziwe na upeo mkubwa wa kufanya uchunguzi kwa mujibu wa majukumu yao.


Waziri wa Utali na Mambo ya Kale, Mudrik Ramadhan Soraga alisema kuwa mkutano huo ni hatua muhimu kwa Zanzibar na Tanzania kuonesha namna ilivyopiga hatua katika kustawisha utawala bora na kusimamia matumizi ya fedha na rasilimali za umma.

Alisema kuwa Zanzibar ipo tayari kupokea wageni na kutoa wito kwa wajumbe wa kongamano hilo kutembelea vivutio vya utalii na uwekezaji viliopo nchini, ili kukuza ushirikiano na uchumi wa Zanzibar na nchi zao.

Mwenyekiti wa SADCOPAC ambaye pia ni Mwenyekiti wa Kamati ya PAC katika Bunge la Zambia, Warren Cisha Wambasi, alipongeza ushirikiano walioupata katika maandalizi ya kongamano hilo linalojumuisha kamati za usimamizi za fedha za umma katika mabunge ya SADC.

Alisema kuwa kamati hizo zina wajibu wa kuhakikisha sheria za matumizi ya fedha na rasilimali za umma zinatekelezwa na kusimamia ipasavyo.

Naye Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) Zanzibar, Dk. Othman Abbas Ali, alieleza kuwa kongamano hilo litatanua wigo wa Ushirikiano baina ya ofisi yake na taasisi za ukaguzi katika eneo la nchi wanachama.




Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi akihutubia wakati akifungua mkutano wa mafunzo ya kuwajengea uwezo wajumbe na wataalamu wa kamati za usimamizi wa fedha za umma kwa nchi wanachama wa jumuiya ya maendeleo ya kusini mwa Afrika (SADCOPAC), jijini Zanzibar jana. **PICHA: IKULU**

# Serikali kutoa huduma ya kifua kikuu magerezani

**Na Mwandishi Wetu**

WIZARA ya Afya Zanzibar kupitia programu shirikishi UKIMWI, homa ya ini, kifua kikuu na ukoma imesema wataendelea kutoa huduma za maradhi ya kifua kikuu katika magereza yote hapa nchini.

Akizungumza juzi katika mkutano uliowakutanisha maofisa wa vyuo vya mafunzo, Kaimu Meneja wa Programu hiyo, Valeria Rashid, alisema katika kuimarisha huduma za kifua kikuu watahakikisha huduma hizo zinawafikia magereza yote kwa lengo la kuwaibua wagonjwa na kuwapatia matibabu ya haraka.

Alisema awali huduma hizo zilikuwa zinatolewa kwa gereza moja ambapo kwa sasa wataweza kutanua huduma hizo kwa magereza yote ya Unguja na Pemba.

Aidha, aliongeza kuwa katika kufanikisha kazi hizo watahakikisha wanajipanga vizuri kwa kukusanya sampuli za makohozi kwa wafungwa wote kwa kuzingatia vigezo kupitia waratibu wa wilaya.

Alisema kufanyika kwa mkutano huo kwa maofisa wa mafunzo utawezesha kutekeleza kazi hizo kwa vitendo kwa lengo la kupambana na maradhi ya kifua kikuu.

Mratibu wa ugonjwa wa kifua kikuu na ukoma Kanda ya Unguja, Dk. Julius Obed Mshana, alisema watu wanaoishi katika mazingira ya mikusanyiko ikiwa ni pamoja na vyuo vya mafunzo wapo katika hatari kubwa ya kuambukizwa na vimelea vya kifua kikuu ukilinganisha na jamii nyingine.

Alisema katika utafiti uliofanyika mwaka 2018 wafungwa 426 waliokuwa katika magereza Zanzibar matokeo yalibaini kuwa wafungwa saba kati ya idadi hiyo walikuwa na ugonjwa wa kifua kikuu.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**LEOCARDIA DOMINICK MAKONDO** anatangaza kupotea kwa kadi ya pikipiki yenye usajili namba **MC116 EAL.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

POLISI TAARIFA:
**PHQ/SHI/KAH/1409/2024**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**ABDALLAH HAMISI NDWATA** anatangaza kupotea kwa kadi ya pikipiki yenye jina **MOHAMMED ENTERPRISES (T) LTD** namba za usajili **MC689CHV** aina ya **BAJAJ BOXER,** CHASSIS NO. **MD2A21BY3KWB89408,** ENGINE NO. **PFZWKB33481.** Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

TAARIFA YA POLISI:
**PHQ/DOD/DOD/12648/2024**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**ANTONY ALOYCE** anatangaza kupotea kwa kadi ya pikipiki yenye jina **FAIR AUTO PVT LIMITED** namba za usajili **MC 848 BVN** aina ya BOXER, Chassis No. **MD2A21BY9HWH91156,** Engine No. **PFZWHH82501.** Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

TAARIFA YA POLISI:
**PHQ/DOD/DOD/11789/2024**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**IVONA AGUSTINO KALENZI** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye majina **BEATUS ALKADO MALEMA** namba za usajili T 914 DPT aina ya **LANDCRUISER**, Chassis No. **JTECB09J603018712,** Engine No. **1HZ0459745.** Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

TAARIFA YA POLISI:
**PHQ/DOD/DOD/13333/2024**

**ROMATIN GENERAL SUPPLIES COMPANY LIMITED**
**(In LIQUIDATION)**
**(P.O. BOX 11214 MWANZA-NYAMAGANA)**
**COMPANY NUMBER 125992**
**NOTICE OF THE GENERAL MEETING**

**NOTICE IS HEREBY GIVEN** to the general public and to all the Members of **ROMATIN GENERAL SUPPLIES COMPANY LIMITED** the general meeting of the company will be held at Golden Parck, Plot No. 45, Butimba Road, **P.O BOX 11214** mwanza on 28th da of April 2024 at 11:00 am onwards.

**AGENDA**

1. To lay before the Members the Members of the accounts of the company showing how he winding up of the company has been conducted and the property of the company has been disposed of; and
2. To discuss any other business that may arise during the meeting.

Date 3rd day of April 2024

Martin Buyanja Chomba
(Liquidator)

**OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.**
**MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz,**
**website: www.ippmedia.com**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA WILAYA MWANGA**
**UTHIBITISHO NA USIMAMIZI WA MIRATHI**
**SHAURI LA MIRATHI NA 6439 YA MWAKA 2024**
**MAOMBI YA BARUA YA USIMAMIZI WA MIRATHI YA**
**MBAZI MOSSES MSEMO....................MAREHEMU**
**HAPPNESS KHATIBU MSEMO.................MUOMBAJI**

**TAARIFA YA KAWAIDA**
**(Kanuni ya 75)**

Watu wote wanaodai kuwa na haki katika mirathi ya marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia mashauri haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa barua ya usimamiaji wa mirathi kwa muombaji aliyeomba hapo juu.

Mapingamizi yoyote kuhusu maombi haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 5 Mwezi Mei, Mwaka 2024.

Imewasilishwa Mwanga leo tarehe 17 Mwezi Aprili Mwaka 2024.

HAKIMU MKAZI MAHAKAMA YA WILAYA MWANGA

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA WILAYA YA MWANGA**
**UTHIBITISHO NA USIMAMIZI WA MIRATHI**
**SHAURI LA MIRATHI NA 6014 YA MWAKA 2024**
**MAOMBI YA BARUA YA USIMAMIZI WA MIRATHI YA**
**FRANK MUZE SARONGE.........................MAREHEMU**
**ROSEANA YOENI MSEMO..........................MUOMBAJI**

**TAARIFA YA KAWAIDA**
**(Kanuni ya 75)**

Watu wote wanaodai kuwa na haki katika mirathi ya marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia mashauri haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa barua ya usimamiaji wa mirathi kwa Muombaji aliyeomba hapo juu.
Mapingamizi yoyote kuhusu maombi haya yawe yameandikwa mnamo au kabla ya tarehe **22 mwezi APRILI, Mwaka 2024**
Imewasilishwa Mwanga leo tarehe 15 mwezi APRILI Mwaka 2024.

HAKIMU MKAZI MAHAKAMA YA WILAYA MWANGA

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA WILAYA YA MWANGA**
**UTHIBITISHO NA USIMAMIZI WA MIRATHI**
**SHAURI LA MIRATHI NA 6085 YA MWAKA 2024**
**MAOMBI YA BARUA YA USIMAMIZI WA MIRATHI YA**
**NEATNESS YOENI MUZE..........................MAREHEMU**
**ROSEANA YOENI MSEMO..........................MUOMBAJI**

**TAARIFA YA KAWAIDA**
**(Kanuni ya 75)**

Watu wote wanaodai kuwa na haki katika mirathi ya marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia mashauri haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa barua ya usimamiaji wa mirathi kwa Muombaji aliyeomba hapo juu.
Mapingamizi yoyote kuhusu maombi haya yawe yameandikwa mnamo au kabla ya tarehe 22 mwezi APRILI, Mwaka 2024
Imewasilishwa Mwanga leo tarehe 15 mwezi APRILI Mwaka 2024.

HAKIMU MKAZI MAHAKAMA YA WILAYA MWANGA

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE N. 6068/ 2024**
**In the matter of the Estate of the late MARY SYLVESTOR MPONELA of Nduka dodoma Within Dodoma Region.**
**AND**
**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION**
**EMMY SYLVESTOR MPONELA**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 Probate Rules Gn. 369 of 163)**

ALL PERSONS claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 18 Day of 4, 2024
Date at Dodoma this 20 Day of MARCH, 2024.

RESIDENT MAGISTRATE

KWA MAHITAJI YA KUTANGAZA SUMMONS, KUPOTEA KWA CHETI, KUPOTEA KWA KADI YA GARI/PIKIPIKI NA USIMAMIZI WA MIRATHI.

TUPIGIE: +255 - 0677 020701

AU

TEMBELEA OFISI ZA MATANGAZO, MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.

E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HABARI KIMATAIFA

# Mafuriko Dubai yaathiri safari za ndege

**Dubai,** U.A.E

MVUA kubwa imenyesha katika baadhi ya mataifa ya Ghuba na kusababisha mafuriko katika eneo hilo.

Mtu mmoja amekufa baada ya gari lake kusombwa na maji huko Ras Al Khaima, kufuatia mafuriko.

Safari za ndege kuelekea uwanja wa ndege wa kimataifa wenye shughuli nyingi zaidi, zilielekezwa kwingine, ingawa zimeanza tena.

**Katika maeneo mengine takriban watu 117,000 wamehamishwa nchini Kazakhstan, kutokana na mafuriko katika taifa hilo la Asia ya Kati.**

Mamlaka nchini Oman, imesema watu 18 wamefariki kutokana na mafuriko.

Mataifa kadhaa yalipata mvua ya takribani mwaka mmoja kwa siku moja.

Video ambayo haijathibitishwa kutoka Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Dubai, ilionyesha ndege zikiacha mawimbi wakati zikishuka kwenye njia za ndege zilizofurika.

Katika maeneo mengine takriban watu 117,000 wamehamishwa nchini Kazakhstan, kutokana na mafuriko katika taifa hilo la Asia ya Kati.

Mafuriko hayo yaliyosababishwa na kuongezeka kwa ujazo wa mto Tobol karibu na mji wa Kurgan kusini mwa Russia, yamefikia viwango vya juu vya tahadhari.

Maafa hayo yamesababishwa na kuyeyuka haraka kwa theluji huku kukiwa na mvua kubwa, jambo linalosababisha kuongezeka kwa ujazo wa mito mikubwa zaidi barani Ulaya.

Nchini Russia, karibu watu 200,000 wamehamishwa pia kutokana na mafuriko hayo. **BBC/DW**



Baadhi ya maeneo yaliyokumbwa na mvua kubwa jijini Dubai, U.A.E. **PICHA: BBC**

## Zelensky ataka NATO iijadili nchi yake

**KYIV,** Ukraine

RAIS wa Ukraine, Volodymyr Zelensky, amesema mjini Kyiv, kwamba anapanga kuitisha mkutano wa Baraza la Jumuiya ya Kujihami NATO na Ukraine.

Anasema lengo ni kutoa wito wa kuimarishwa ulinzi wa anga ya nchi yake.

Akilinganisha hali ya Ukraine na ile ya Israel, baada ya shambulizi kubwa la Iran la makombora na droni kuzuiwa mwishoni mwa wiki;

Zelensky alisema Ukraine itaomba kupewa mifumo ya ulinzi wa mashambulizi ya angani na makombora.

Alisema Waukraine wana haki ya kulindwa dhidi ya ugaidi.

Rais huyo wa Ukraine, alimpongeza Kansela wa Ujerumani Olaf Scholz, kwa kutafuta suluhisho la mzozo huo.

Akizungumza na Rais wa China Xi Jinping, mjini Beijing jana, Scholz alisisitiza umuhimu wa China kwenye jukwaa la kimataifa.

Kama mshirika muhimu wa Russia, Xi anaonekana kuwa na ushawishi kwa Rais wa Russia, Vladmir Putin.

Zelensky alisema China inaweza kusaidia kurejesha amani nchini Ukraine na utulivu katika uhusiano wa kimataifa.

Uswisi itakuwa mwenyeji wa mkutano wa kilele wa amani katikati ya mwezi Juni, ambao China imealikwa.**DW**



## Iran; Hatushiriki mzozo, tuna haki kujilinda

**DAR ES SALAAM,** Tanzania

JAMHURI ya Kiislamu ya Iran, imetoa msimamo wa kutumia haki ya kujilinda kiasili chini ya Sheria ya Kimataifa.

Imesema kwamba haifanyi kazi ya kuongeza au kusambaza mgogoro, ikionya kuhusu machafuko zaidi ya kijeshi yanayoweza kusababishwa na utawala wa Israel.

Hayo yamebainishwa katika taarifa ilitolewa jana, kwa vyombo vya habari na Serikali ya Iran, kupitia Mtaalamu wa Ushauri wa Kitamaduni wa Ubalozi wa Iran nchini Tanzania, Maulid Sengi.

"Tunatoa msimamo wa Jamhuri ya Kiislamu ya Iran kuhusu kutumia haki yake ya kujilinda kiasili chini ya Sheria ya Kimataifa kujibu mashambulizi ya Kijeshi ya Utawala wa Israel, dhidi ya majengo ya kidiplomasia ya Iran huko Syria.

"Jamhuri ya Kiislamu ya Iran, inarudia msimamo wake thabiti kwamba haifanyi kazi ya kuongeza au kusambaza mgogoro katika eneo, inaonya kuhusu machafuko zaidi ya kijeshi yanayoweza kusababishwa na utawala wa Israel.

"Iran inathibitisha tena azma yake isiyo na shaka ya kulinda watu wake, usalama wa kitaifa na maslahi, uhuru na utegemezi wa eneo dhidi ya tishio lolote au vitendo vya uvamizi na kujibu vitisho au uvamizi huo kwa nguvu na kulingana na sheria ya kimataifa," alisema.

Alisema, Iran haina nia ya kushiriki katika mzozo na Marekani katika eneo hilo, ikiwa Marekani itaanzisha operesheni za kijeshi dhidi ya Iran, raia wake au maslahi yake, itaendelea kutunza haki yake ya asili ya kujibu kwa kipimo.

Taarifa hiyo ilisema kwamba katika mazungumzo ya simu na Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa, Aprili 2, Waziri wa Mambo ya Nje wa Iran, Hussein Amirabdollahian alijadili hali hiyo na kutaka hatua sahihi zichukuliwe na kulaani kwa nguvu kutoka kwa jamii ya kimataifa na Baraza la Usalama, kwa uhalifu huo wa kutisha.

"Katika barua zetu zilizotumwa kwa Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa na Katibu Mkuu (S/2024/281-5/2024/305), tumesisitiza kuwa shambulio la kigaidi la Israeli dhidi ya majengo ya kidiplomasia ya Iran huko Damascus;

'Lilikuwa ukiukaji dhahiri wa Sheria ya Kimataifa ya Mkataba wa Umoja wa Mataifa, hasa Ibara ya 2 (4) ya Mkataba na uhuru, uhuru na utegemezi wa kieneo wa Jamhuri ya Arabuni ya Syria.

"Hatua hiyo isiyo halali inawakilisha uvunjaji mbaya wa kanuni msingi na iliyokubaliwa ulimwenguni ya kutotaka kuvunjika kwa wawakilishi na majengo ya kidiplomasia na konsulari, ambayo ni msingi wa uhusiano wa kimataifa," alisema.

Alisema Jamhuri ya Kiislamu ya Iran, ililitaka Baraza la Usalama, kukemea vikali kitendo cha jinai na kuchukua hatua thabiti na sahihi za kuwafikisha watekelezaji kwenye sheria haraka na kuzuia kurudiwa kwa uhalifu kama huo, dhidi ya majengo ya kidiplomasia ya mwanachama yeyote.

"Kama mwanachama anayehusika wa Umoja wa Mataifa, Jamhuri ya Kiislamu ya Iran, inajitolea kwa madhumuni na kanuni zilizoorodheshwa katika Mkataba wa Umoja wa Mataifa na inathibitisha kujitolea kwake kwa kudumisha amani na usalama wa kimataifa.

Alisema April 13, mwaka huu, vikosi vya kijeshi vya Jamhuri ya Kiislamu ya Iran, vilifanya mashambulizi ya kijeshi dhidi ya malengo ya kijeshi ya Israel, kwa kutumia makombora na ndege zisizo na rubani.

Jamhuri ya Kiislamu ya Iran, imewajulisha Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa, juu ya vitendo vya Israel pamoja na haki ya asili ya Iran, chini ya sheria ya kimataifa ya kujibu mashambulizi ya kigaidi kama hayo (A/78/838-5/2024/281).

# WACHEZAJI, YANGA, AZAM WAFUNIKA REKODI LIGI KUU

**Na Adam Fungamwango**

WACHEZAJI wa timu za Yanga na Azam wametawala katika rekodi za Ligi Kuu Tanzania Bara kila kona, wakiwaacha mbali wachezaji wa timu zingine, ikiwamo Simba ambayo haina mchezaji yeyote aliyechomoza kuongoza.

**Kwa mujibu wa takwimu mpya zilizotolewa jana na Bodi ya Ligi, na za Dawati la Michezo la Nipashe, wachezaji wa timu hiyo wameonekana kufunika kila kona, kuongoza kwa ufungaji, kutoa pasi za mwisho na jumla ya mabao waliochangia kwenye timu zao.**

Katika eneo la orodha ya wafungaji mabao, Stephane Aziz Ki wa Yanga anaongoza akiwa amepachika mabao 14, huku Kipre Junior wa Azam, akiwa kinara kwenye pasi za mwisho zilizozaa mabao. 'asisti' akiwa nazo nane mpaka sasa.

Beki wa kulia wa Yanga, Yao Kouassi, anaongoza kwa 'asisti' upande wa mabeki, akiwa nazo saba mpaka sasa na akishika nafasi ya pili, nyuma ya Muivory Coast mwenzake, Kipre.

Wakati Mburkina Faso, Aziz Ki akiongoza kwenye orodha ya wafungaji, anafuatiwa na mchezaji wa Azam FC, Feisal Salum 'Fei Toto', ambaye ana mabao 13, waziri Junior wa KMC akiwa na mabao 11, Maxi Nzengeli, pia wa Yanga akiwa na tisa.

Jumla ya wachezaji watano wamefunga mabao manane kila mmoja, ambao ni Mudathir Yahaya wa Yanga, Kipre wa Azam, Samson Mbangula wa Prisons, Marouf Tchakei wa Ihefu na Jean Baleke wa Simba.

Upande wa 'asisti' za jumla ambako Kipre wa Azam anaogoza, anafuatiwa na Kouassi na Aziz Ki wote wa Yanga ambao kila mmoja ana 'asisti' saba, huku Fei Toto wa Azam akiwa nazo sita. Kwa upande wa uchangiaji mabao, Aziz Ki bado amefunika akiwa amechangia mabao 21 katika timu yake, yaani mabao yake 14 ya kufunga jumlisha na 'asisti' zake saba, na anafuatiwa kwa mara nyingine tena na mchezaji wa Azam, Fei Toto ambaye ameichangia timu yake mabao 19, ikiwa ni mabao yake 13 aliyofunga na 'asisti' zake sita alizotoa kwa wenzake.

Hata hivyo, wachezaji wa Azam FC, wanaweza kubadili takwimu hizi na kujiongezea rekodi za mabao na 'asisti', kwani jana usiku ilitarajia kucheza dhidi ya Mashujaa FC, Uwanja wa Azam Complex, Chamazi, Dar es Salaam.

Sehemu pekee ambayo wachezaji wa Yanga na Azam wamepigwa bao ni kwenye 'clean sheets' za makipa, ambapo Ley Matampi wa Coastal Union, bado ameendelea kukomaa kileleni akiwa nazo 10 mpaka sasa.

Hata hivyo, anakaribiwa na kipa wa Yanga, Djigui Diarra ambaye amekaa mechi tisa langoni bila kuruhusu bao.

Wengine ni John Noble wa Tabora United na Costantine Malimi wenye 'clean sheets' saba kila mmoja, Jonathan Nahimana wa Namungo, yeye ananzo sita pamoja na Yona Amosi wa Prisons, Ayoub Lakred wa Simba, Ramadhani Chalamanda wa Kagera Sugar na Wilbol Maseke wa KMC wana 'clean sheets' tano kila mmoja.

## *Tembo Warriors yakerwa michuano Afrika kusogezwa*

**Na Shufaa Lyimo**

MASHINDANO ya Kombe la Afrika ya mpira wa miguu kwa watu wenye ulemavu yaliyokuwa yafanyike jijini Cairo, Misri kuanzia kesho, sasa yamesogezwa mbele mpaka Mei 19, mwaka huu, huku Timu ya Taifa ya Tanzania, Tembo Warriors ikishuka dimbani Mei 20 kuvaana na Rwanda.

Katika mashindano hayo ambayo ni ya kuwania kufuzu michuano ya Kombe la Dunia kwa wenye ulemavu itakayofanyika mwaka 2026 jijini Paris, Ufaransa, Tanzania imepangwa Kundi D na ya Sierra Leone, Angola pamoja na Rwanda.

Akizungumza na Nipashe jana, Meneja wa Tembo Warriors, Zaharani Mwenemti, alisema mashindano hayo yamesogezwa mbele kutokana na baadhi ya nchi kutokamilisha visa zao.

"Mashindano yamesogezwa mbele mpaka mwezi ujao kutokana na baadhi ya nchi kushindwa kukamilisha visa, pia ninchi 10 pekee ndio zilithibitisha kushiriki, hivyo ikalazimika yasogezwe mbele," alisema Mwenemti.

Alisema kwa upande wao taarifa hiyo imewaathiri wachezaji kwani walikuwa wamefanya maandalizi ya kutosha kuelekea kwenye mashindano hayo, ambapo walipata nafasi ya kucheza michezo mingi ya kirafiki walipokuwa kambini Karatu, Arusha.

Meneja huyo alisema mara baada ya kupata taarifa hiyo, serikali imelazimika kuvunja kambi waliyokuwa wameiweka Karatu mkoani Arusha na kuihamishia kwenye shule ya Filbert Bayi mkoani Kibaha.

Naye nahodha wa timu hiyo, Juma Kidevu, alisema taarifa hiyo imewaathiri kwa kuwa tayari walikuwa wamejiandaa na mchezo wao huo.

**PASUA NJIA...**



Mchezaji wa timu ya Bulls, Ben Mango, akijaribu kumtoka mchezaji wa timu ya Champion Football Club ya Kawe, walipokutana kwenye mchezo wa kirafiki katika Uwanja wa Soccer Point, Mikocheni, Dar as Salaam juzi. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## KMKM, KVZ FC zapania fainali FA Cup

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

WAKATI zikishuka dimbani leo kwenye hatua ya 16-bora ya michuano ya Kombe la Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF), maarufu FA Cup, timu ya KMKM SC na KVZ FC, zimeweka malengo ya kuhakikisha zinatinga fainali, huku kila moja ikieleza nia yake ya kutwaa kombe hilo.

Timu hizo za Ligi Kuu Zanzibar leo zitashuka katika viwanja viwili tofauti kuvaana na wapinzani ambapo katika Uwanja wa Mau A timu ya KVZ FC itawaalika Raskazone FC wakati Uwanja wa Mau B, KMKM itawaalika Paje Star FC, michezo yote ikichezwa saa kumi alasiri.

Kuelekea michezo hiyo makocha wa timu kutoka Ligi Kuu, KMKM na KVZ FC, kila mmoja ameweka wazi kuwa malengo yao makubwa ni kuhakikisha anatwaa taji la mashindano hayo.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha wa KMKM, Ame Msimu, alisema matarajio yake kwanza ni kuhakikisha wanafika hatua ya fainali ya michuano hiyo na kisha kubeba kombe hilo.

Alisema timu yake imekuwa haifanyi vizuri katika michuano ya kombe hilo kwa kuishia hatua za awali ya 32, lakini msimu huu wamedhamiria kuhakikisha wanavuka hatua zote.

"Tunataka ubingwa wa michuano hii ya ZFF, tunataka msimu huu tufanikiwe lengo la kutwaa kombe hili kama tulivyofanikiwa kufika hatua hii ya 16, nina imani pia tutafanikiwa kufika fainali," alisema.

Naye Kocha wa KVZ FC, Ali Mohmmed Ameir, alisema mchezo wao dhidi ya Raskazone si rahisi kama unavyotajwa na wengi.

Alisema anauchukulia kwa makini mchezo huo ili kufanikisha malengo ya kusonga mbele katika michuano hiyo migumu.

"Ugumu wa mashindano haya hayana nafasi ya pili maana ukifungwa ndio umetoka, ndio maana kila hatua tunayoingia bila kuangalia timu ya kukutana nayo tunauchukulia kwa uzito mchezo huo," alisema.

Hata hivyo, alisema anaamimi maandalizi waliyofanya wachezaji wake yatasaidia kufanya vizuri katika michuano hii na hata kufikia hatua ya fainali.

## ZISIKUPITE

### WILLIAMS AFUATILIWA SPURS

KLABU ya Tottenham Hotspur inamfuatilia mshambuliaji wa Athletic Bilbao, Nico Williams, 21, ambaye ana kipengele cha kuruhusiwa kuondoka kwa pauni milioni 42.8 katika mkataba wake. ***(Telegraph)***

### JOELINTON MKATABA MPYA

MAZUNGUMZO ya Newcastle United na kiungo wa kati wa Brazil, Joelinton, 27, yanaendelea vema na mchezaji huyo anakaribia kusaini mkataba mpya na klabu hiyo ya Tyneside. ***(Telegraph)***

### VARANE SASA KUUZWA

MLINZI Raphael Varane, 30 na kiungo wa kati wa Brazil Casemiro (32), wanatarajiwa kuongoza orodha ya wachezaji ambao Manchester United itawauza msimu wa majira ya joto.***(Talksport)***

### PAGUETA MAMBO BADO

KLABU ya Manchester City iaweza kutumia vema nia ya Lucas Paqueta ya kuondoka West Ham msimu ujao - lakini iwapo tu uchunguzi wa FA kuhusu madai ya ukiukaji wa kanuni za kamari uliofanywa kwa kiungo huyo wa kati wa Brazil mwenye umri wa miaka 26, utatupiliwa mbali. ***(Guardian)***

### MUSIALA ATAKIWA CITY

MANCHESTER City ipo tayari kutumia pauni milioni 120 kumsajili mshambuliaji wa Ujerumani, Jamal Musiala mwenye umri wa miaka 21, kutoka Bayern Munich. ***(TeamTalk)***

### EDWARDS AWANIWA LIVER

LIVERPOOL inatayarisha uhamisho wa msimu wa majira ya joto kwa ajili ya mshambuliaji wa Sporting Lisbon, Marcus Edwards, 25, na mlinzi wa Ureno, Goncalo Inacio, 22. ***(Football Insider)***

### ALMIRON, WILSON KUONDOKA

MSHAMBULIAJI wa Paraguay, Miguel Almiron, 30 na mshambuliaji wa England, Callum Wilson, 32, ni miongoni mwa wachezaji ambao wanaweza kuondoka Newcastle United huku klabu hiyo ikijiandaa kwa ujenzi wa majira ya joto. ***(Telegraph)***

### ADARABIOYO MKATABA MPYA

KLABU ya Manchester United na Tottenham Hotspur zimewasiliana na beki wa kati wa Fulham, Tosin Adarabioyo, 26, katika kujaribu kufikia makubaliano ya awali ya mkataba mpya na mchezaji huyo. ***(TeamTalk)***

### WAN-BISSAKA AWANIWA

AARON Wan-Bissaka, 26, wa United analengwa kwa pauni milioni 13 na Inter Milan huku beki huyo wa England, akimaliza mkataba wake mwishoni mwa msimu wa 2025. ***(Gazetta dello Sport)***

### GALLAGHER HUYOOO SPURS

KLABU ya Tottenham Hotspur inatumaini kukamilisha mkataba wa haraka kwa ajili ya kumnunua kiungo wa kati wa Chelsea, Conor Gallagher, 24, dirisha la uhamisho litakapofunguliwa. ***(Sun)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# MBAPPE: NAUTAKA UBINGWA WA UEFA

**BARCELONA,** Hispania

## Nina ndoto ya kushinda Ligi ya Mabingwa Ulaya nikiwa hapa Paris...

MSHAMBULIAJI wa Paris Saint-Germain, Kylian Mbappe, amesema kuisaidia klabu yake ya nyumbani kushinda taji lao la kwanza la Ligi ya Mabingwa Ulaya ni jambo la kujivunia kwake, kauli hiyo akiitoa baada ya kufunga mabao mawili na kuiwezesha timu yake kuibuka na ushindi wa mabao 4-1 dhidi ya Barcelona na kutinga nusu fainali juzi, Jumanne.

Mbappe, ambaye anatazamiwa kuondoka PSG katika majira ya joto kujiunga Real Madrid, aliwaambia waandishi wa habari kwamba mustakabali wake haupo akilini mwake na kwamba analenga kabisa kuleta utukufu katika mji mkuu wa Ufaransa.

"Nina ndoto ya kushinda Ligi ya Mabingwa Ulaya nikiwa hapa Paris," alisema Mbappe, akiwaambia waandishi wa habari katika uwanja wa Olimpiki wa Barcelona Jumanne.

**"Ninajivunia kuwa PSG tangu siku ya kwanza. Si kwa sababu kuna nyakati nzuri na mbaya ambazo fahari yangu inapata pigo. Fahari ya kuichezea klabu hii na kuwakilisha klabu ya mji mkuu wa nchi yangu ni kitu maalum kwa ajili yangu.**

"Kujionea jioni kama hii kama mchezaji wa Paris ni vema. Tuna hatua moja zaidi ya kufanya kabla ya kufika fainali huko Wembley, kwa hiyo tunahitaji kuwa watulivu."

Baada ya kufungwa mabao 3-2 katika mechi ya kwanza mjini Paris, PSG walitoka nyuma kwa bao 1-0 wakiwa Barcelona baada Ronald Araujo kutolewa kwa kadi nyekundu kwa kumchezea vibaya Bradley Barcola.

Mshambuliaji wa zamani wa Barcelona, Ousmane Dembele aliwasawazishia wageni kabla ya kipindi cha mapumziko huku Vitinha na Mbappe wakimaliza kazi kipindi cha pili, ambapo sasa PSG itavaana na Borussia Dortmund katika nusu fainali baada ya timu hiyo ya Bundesliga kuishinda Atletico Madrid.

HABARI MICHEZO



# GUNDOGAN ALAUMU BARCA KUTOLEWA

**BARCELONA,** Hispania

ILKAY Gundogan alilaumu makosa binafsi wakati Barcelona ikitolewa kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya juzi, Jumanne, akisema mabingwa hao wa Hispania waliwapa Paris Saint-Germain mchezo rahisi.

Barca waliongoza kwa mabao 3-2 kutoka mchezo wa mkondo wa kwanza kule Paris na kutoa faida ya mabao wakati Raphinha alipowapatia uongozi wa dakika ya 12 kwenye Uwanja wa Olympic.

Hata hivyo, mchezo uliyumba baada ya nusu saa ambapo Ronald Araujo alitolewa nje kwa kadi nyekundu kwa kumchezea rafu Bradley Barcola, huku PSG wakiibuka na ushindi wa mabao 4-1 usiku huo, na kusonga mbele kwa jumla ya mabao 6-4, hivyo kutinga nusu fainali dhidi Borussia Dortmund.

"Nimesikitishwa sana kwa sababu tulikuwa katika nafasi nzuri, si tu baada ya mechi ya kwanza, lakini kufungua bao la kwanza pia," alisema Gundogan akiiambia CBS.

"Kila kitu mikononi mwetu na tulitoa kwa njia rahisi zaidi. Tuliitoa PSG na ndiyo sehemu ya kukatisha tamaa zaidi.

"Usipoipata, na sijui kama aliipata, ukae pembeni. Napendelea golini pale au kumwacha mchezaji mmoja, ingawa alicheza mbele kabisa, kwa hiyo sijui kama angeufikia mpira, lakini acha kipa apate nafasi ya kutuokoa au hata goli.

"Kupata kadi nyekundu, kumshusha mchezaji mapema, inaua mchezo."

"Vitendo vya maamuzi, hali muhimu, vitakutuza au kukuadhibu," Gundogan alisema. "Kwa bahati mbaya kwa usiku wa leo walituadhibu."



# Bellingham alia ubaguzi wa rangi

**MADRID,** Hispania

JUDE Bellingham amesema Vinicius Junior na wachezaji wengine weusi wanahitaji kuungwa mkono zaidi katika kushughulikia "tatizo kubwa" la ubaguzi wa rangi katika soka la Hispania, akielezea unyanyasaji ambao baadhi ya wachezaji hupokea kama "chukizo."

Picha za runinga zilionesha shabiki akitoa ishara za kibaguzi kuelekea kwa mchezaji mwenzake, Aurelien Tchouameni baada ya kufunga bao katika ushindi wa 1-0 wa LaLiga Jumamosi dhidi ya Real Mallorca, huku wenyeji wakisema wanafanya kazi na polisi kubaini mtu aliyehusika.

Vinicius amekuwa akilengwa kwa dhuluma za ubaguzi wa rangi na mashabiki wa upinzani mara nyingi, ikiwa ni pamoja na wakati wa mchezo wa ligi ugenini dhidi ya Valencia msimu uliopita ambao ulizua malalamiko ya kimataifa kuhusu suala hilo.

"Hata sikujua kuhusu tukio la Tchouameni," alisema Bellingham alipoulizwa kuhusu tatizo hilo wakati wa mkutano na waandishi wa habari Jumanne.

"Katika mechi tunapoenda ugenini kwenye LaLiga, unakaribia kuzoea kiasi kwamba hata sikujua tukio hilo. Hilo ni tatizo kubwa.

"Mengi zaidi yanapaswa kufanywa, iwe ni adhabu au jinsi unavyoitikia, au jinsi unavyosonga kwa kasi. Ni njia mbaya kwa mchezaji kujiandaa kwa mchezo, akijua labda atanyanyaswa. Inachukiza, haipaswi kutokea watu walio madarakani wanahitaji kufanya zaidi, hasa kwa Vini.

# Martial kuondoka Man Utd

**Manchester,** ENGLAND

MSHAMBULIAJI wa Manchester United, Anthony Martial, huenda akapata nafasi ya kufufua makali yake, endapo atafanikiwa kuondoka Old Trafford.

Martial amekuwa na wakati mgumu wa kutumika kwenye kikosi cha kwanza cha Manchester United, majeraha ya mara kwa mara, hali ambayo inamnyima nafasi ya kurejea katika kiwango chake kama alichokua nacho klabuni hapo mwaka 2015.

Mabingwa wa zamani wa Italia Juventus wanatajwa kuwa kwenye mpango wa kumsajili mshambuliaji huyo mwenye umri wa miaka 28, mwishoni mwa msimu huu, na inaaminiwa endapo dili hilo litakamilishwa basi Martial atapata nafasi ya kucheza mara kwa mara.

Mkataba wa sasa wa Martial utafikia tamati mwishoni mwa msimu huu wa 2023/24, na dili lake la kuondoka Old Trafford litainufaisha Juventus, kwani itampata kama mchezaji huru.

Mtandao wa Tuttosport umeeleza kuwa mabosi wa Juventus wameshawishiwa kumsajili mshambuliaji huyo, huku Benchi la Ufundi la Juventus likiamini ataweza kuwasaidia katika harakati zao za kurejesha ufalme wa soka nchini Italia kuanzia msimu ujao.

Martial pia anatajwa pia kuwaniwa na Klabu ya Tottenham inayonolewa na Kocha Mkuu kutoka nchini Australia, Ange Postecoglou.

Hata hivyo, klabu hiyo yenye maskani yake makuu Kaskazini mwa Jiji la London, huenda ikazidiwa ujanja na Juventus, inayopewa nafasi kubwa kumsajili mshambuliaji huyo.



## Yanga kuivaa Tabora United robo fainali FA

Na Saada Akida

DROO ya robo fainali ya Kombe la Shirikisho la Benki ya CRBD (CRDB Federation Cup), imefanyika jana ambapo bingwa mtetezi wa michuano hiyo Yanga, atamkaribisha Tabora United katika mchezo utakaochezwa Uwanja wa Azam Complex uliopo Chamazi Dar-es-Salaam.

Michezo mingine ni Azam FC wakiwa nyumbani wataikaribisha Namungo FC katika dimba hilo la Azam, Coastal Union dhidi ya Geita Gold FC Uwanja wa Mkwakwani jiji Tanga na Ihefu FC watakuwa nyumbani dhidi ya Mashujaa FC, Uwanja wa Liti mkoani Singida.

Michezo hiyo ya robo fainali inatarajiwa kuchezwa kati Mei 2 hadi 4, huku nusu fainali ikitarajiwa kuchezwa Mei 18 hadi 19 na fainali itapigwa Juni 2, mwaka huu.

Nusu fainali ya kwanza itachezwa kati ya mshindi wa mchezo kati ya Azam FC dhidi ya Namungo FC atacheza na mshindi kati ya Coastal Union dhidi ya Geita Gold FC.

Kwa upande wa nusu fainali ya pili itakuwa kati ya mshindi wa Ihefu FC dhidi ya Mashujaa FC kati ya mshindi wa mechi ya Yanga na Tabora United.

Kwa mujibu wa Meneja wa Mashindano ya Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF), Baraka Kizunguto, nusu fainali ya kwanza ya itachezwa Uwanja wa CCM Kirumba jijini Mwanza huku wakisubiri taratibu zingine juu ya uwanja utakaochezwa nusu fainali ya pili

"Fainali itachezwa Manyara katika Uwanja wa Tanzanite Kwaraa, timu zote zinazocheza robo fainali zinatakiwa kujiandaa," alisema Kizunguto.

# UHAMIAJI FC: TUTARUDI LIGI KUU NA KASI MPYA

Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR

TIMU ya Uhamiaji FC imesema matarajio na mipango yao ya kumaliza nafasi nne za juu katika msimamo wa Ligi Kuu Zanzibar msimu huu, yanategemea zaidi kufanya vizuri michezo 10 ya ligi hiyo ambayo inatarajiwa kuendelea Aprili 27, mwaka huu, baada ya kusimama kwa muda.

Uhamiaji FC ni miongoni mwa timu ambazo zimevuna alama moja moja mara nyingi kutokana na kupata sare 10 katika mzunguko wa kwanza wa ligi hiyo.

**Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Abdisaleh Abdallah, alisema baada ya kutopata matokeo ya kuridhisha karibia nusu ya michezo waliyocheza msimu huu, michezo iliyobakia wamejipanga kuhakikisha wanashinda ili kuiweka timu yao katika nafasi za juu kwenye msimamo wa ligi hiyo.**

Alisema katika kuhakikisha wanatimiza ndoto yao hiyo, kwa sasa baada ya kumaliza mfungo wa Ramadhani ameandaa programu maalum ya kuwajenga kimwili wachezaji wake 'fitness' kutokana na mapumziko ya muda mrefu waliyoyapata.

Alisema mpango huo unalenga kuwarejesha mchezoni wachezaji pamoja na kuyanfanyia kazi mapungufu waliyoyaona katika michezo iliyopita.

Alisema eneo kubwa ambalo watalifanyia kazi ni nafasi ya ushambuliaji pamoja na mabeki wa kulia kwa kuwa idara hizo mara kwa mara zimekuwa zikifanya makosa yanayojirudia.

"Tunarudi na kasi kubwa, kasi ambayo tunataka kufanikisha lengo letu la kunyakuwa alama tatu katika kila mchezo ambao tunashuka uwanjani," alisema.

Aidha, alisema katika mchezo wao wa kirafiki dhidi ya Klabu ya Simba, waliweza kupata mbinu mpya ambazo watazitumia vizuri hasa kwa upande wa washambuliaji na walinzi.

Alisema anaamini kupitia mchezo huo wa kirafiki na michezo kadhaa waliyocheza itawasaidia katika kufanikisha lengo lao la kupata matokeo ya ushindi katika mechi 10 zilizobaki.

Timu ya Uhamiani FC ipo nafasi ya saba ikiwa na alama 28, katika michezo 20 iliyocheza hadi sasa katika ligi hiyo ikiwa imeshinda mechi sita, sare 10 na kufungwa mara nne.

KAZI INAENDELEA...



Wachezaji wa Simba wakiendelea na mazoezi visiwani Zanzibar walipoweka kambi kujianda na mechi ya 'Derby' ya Kariakoo dhidi ya Yanga itakayopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa keshokutwa, Jumamosi. **PICHA: SIMBA**

## *Pacome fiti 100% kuitumikia Yanga*

INATOKA UKURASA 24

mchezo wa hatua ya 16-bora ya Kombe la Shirikisho, FA Cup dhidi ya Dodoma Jiji wakishinda mabao 2-0 na kutinga hatua ya robo fainali.

Pia, ilicheza mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Singida Fountain Gate na kuibuka na ushindi wa mabao 3-0, mchezo uliochezwa Uwanja wa CCM Kirumba jijini Mwanza.

Katika hatua nyingine, uongozi wa Klabu ya Azam FC, umethibitisha kupeleka ofa Klabu ya Yanga ukionyesha nia ya kumtaka mshambuliaji wao, Clement Mzize.

Akithibitisha taarifa hiyo jana, Msemaji wa timu ya Azam FC, Thabit Zakaria 'Zaka za Kazi', alisema wamelazimika kupeleka ofa hiyo baada ya kuridhishwa na kiwango cha mshambuliaji huyo, huku wakieleza kwa sasa hawana mshambuliaji asilia katika timu yao.

"Ni kweli tumepeleka ofa Yanga ya kumhitaji Mzize isipokuwa mpaka sasa bado hatujajibiwa endapo kama tutakubaliwa tutakaa meza moja na kufanya biashara kwa kuwa Yanga tulifanya nao biashara muda mrefu wakati tunamhitaji Mrisho Ngassa na iliwezekana," alisema Zaka za Kazi.

Alisema wameamua kumtafuta huduma ya Mzize kwa ajili ya kupanga mikakati kuelekea msimu ujao wa Ligi Kuu Tanzania Bara, ambapo usajili utaanza mapema mwezi Juni mwaka huu.

Aidha, alisema hawamlazimishi aliyekuwa mshambuliaji wao, Prince Dube, kuichezea timu hiyo na badala yake anapaswa kufuata taratibu za mkataba ili wamruhusu aendelee na maisha yake.

"Kuna ofa ambazo zilitumwa na Klabu ya Simba pamoja na Al Hilal ya Sudan, zikionyesha nia ya kumhitaji baada ya muda mfupi tutatoa taarifa ya hizo ofa ili Watanzania pamoja na mashabiki wetu wafahamu kinachoendelea," alisema.

## Simba yaipania Yanga

INATOKA UKURASA 24

kubwa analoliona ni umaliziaji tu hakuna kingine, akaenda mbali zaidi akisema ni tatizo la nchi nzima, kwani ameangalia hata baadhi ya mechi za ligi na kugundua udhaifu wa washambuliaji wengi wanaocheza soka nchini.

"Tunafanya kila kitu, lakini hatuweki mpira wavuni, hii ni shida, nimeamua kubadilisha kidogo mbinu na mfumo ili kuwarahishia kazi ya kufunga, siku hizi chache ambazo tupo hapa nawafua wachezaji wangu ili wawe makini wanapokuwa mbele ya lango," alisema Benchikha raia wa Algeria.

Timu hizo zinakwenda kucheza mechi ya 'dabi', Yanga ikiwa inaongoza ligi kwa pointi 55 ambayo itakuwa mwenyeji wa mchezo huo, huku Simba, inayoshika nafasi ya tatu kwa pointi 46, ikiwa mgeni kwenye mechi hiyo itakayopigwa Jumamosi kuanzia saa 11:00 jioni.

# Michezo

Alhamisi Aprili 18, 2024

Nipashe




Bellingham alia na ubaguzi UKURASA 22

NUSU FAINALI HIYOOO...




Mshambuliaji wa Paris Saint-Germain, Kylian Mbappe, akishangilia baada ya kuifungia timu yake moja kati ya mabao mawili aliyofunga wakati wakishinda 4-1 dhidi ya Barcelona kwenye mechi ya robo fainali mkondo wa pili ya Ligi ya Mabingwa Ulaya na kutinga nusu fainali. Mechi hiyo ilipigwa Uwanja wa Olimpiki wa Barcelona juzi, Jumanne. **Habari Uk.21. PICHA: MTANDAO**

# Pacome fiti 100% kuitumikia Yanga

**Saada Akida na Shufaa Lyimo**

## ●●● Gamondi kuamua Jumamosi, Azam FC nayo sasa yamtaka Mzize...

ZIKIWA siku mbili kabla ya mechi ya 'Derby' ya Kariakoo, Kiungo Mshambuliaji wa Yanga, Pacome Zouzoua, ameanza mazoezi ya ushindani na wachezaji wenzake baada ya kukaa nje ya uwanja kwa siku 29 akiuguza jeraha la nyama za paja.

**Yanga itaikaribisha Simba kwenye Derby ya Kariakoo, keshokutwa, Jumamosi katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, ikiwa ni mechi ya raundi ya pili ya Ligi Kuu Tanzania Bara.**

Nyota huyo raia wa Ivory Coast, aliumia katika mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Azam FC, uliochezwa Mei 17, mwaka huu, katika Uwanja wa Benjamin Mkapa Dar es Salaam, Yanga wakikubali kichapo cha mabao 2-1.

Akizungumza na Nipashe jana, Daktari wa Yanga, Moses Etutu, alisema Pacome amerejea kwenye uwanja wa mazoezi na anaendelea vizuri katika mazoezi ya ushindani na wenzake.

Alisema awali nyota huyo alikuwa na program maalum ya mazoezi yake binafsi kwa siku alizopewa lakini kwa sasa amerejea uwanjani na kuendelea na majukumu yake ndani ya timu hiyo kama kawaida.

"Pacome tayari ameanza mazoezi na wenzake, kuhusu kumtumia katika mchezo ijao hiyo ni kazi ya benchi la ufundi, kumpa nafasi au kuendelea kumsubiri na kumpa dakika chache za kucheza kwa ajili ya kuwa fiti zaidi," alisema Daktari huyo.

Ofisa habari wa Yanga, Ali Kamwe, alisema nyota huyo ameanza kufanya mazoezi lakini hakuna ulazima wa kocha wa timu hiyo Miguel Gamondi, kulazimika kumtumia kwa mechi ya Derby ya Kariakoo.

"Wachezaji wetu ambao walikuwa majeruhi wameanza kupona na kurudi uwanjani, akiwamo Pacome, lakini hatuwezi kulazimisha mchezaji aliyetoka kwenye majeraha kumpanga kucheza katika mechi kubwa na ngumu kama hii dhidi ya Simba," alisema Kamwe.

Kiungo huyo baada ya kuumia, Yanga imecheza michezo minne, miwili ya Ligi ya Mabingwa wakitolewa na Mamelodi Sundowns ya Afrika Kusini kwa penalti 3-2 baada ya kusuluhu katika michezo yote miwili ya nyumbani na ugenini.

Baada ya hapo Yanga ilicheza

INAENDELEA UKURASA 23

# Simba yaipania Yanga Jumamosi

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI mechi ya watani wa jadi inakaribia, kikosi cha Simba kinaendelea kujifua mjini Zanzibar, huku silaha ya viongozi wa timu hiyo kwa sasa ikiwa ni kuwa kimya, lakini wakiwa kwenye mikakati mikali kuhakikisha inashinda.

Hayo yakiendelea, Kocha Mkuu, Abdelhak Benchikha, amesema kazi yake ya siku hizi mbili tatu ni kuwaweka vizuri wachezaji wake kisaikolojia na kuwapa mbinu mbalimbali za kumalizia mipira kwa kuiweka ndani ya nyavu ili kuibuka kidedea Jumamosi ijayo kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Habari kutoka ndani ya klabu hiyo, zinasema viongozi wa klabu wanaelewa kila kitu kinachoendelea kuwa waandishi wa habari, wachambuzi na hata mashabiki wa soka wanaipa nafasi kubwa Yanga, huku wakiibeza timu yao, na hilo limewapa nafasi ya kukaa kimya bila kuongea neno lolote, lakini wakiwa kwenye mikakati mbalimbali kuhakikisha wanashinda mechi hiyo na kujiongezea pointi tatu.

"Mikakati inayofanywa ni kuzuia hila na mbinu zozote chafu ambazo zinaweza kutumika ili kupoteza mechi, kwa sababu wanaamini hata mechi iliyopita hawakufungwa mabao 5-1 kwa kuzidiwa sana na watani zao, ila kuna mbinu ambazo walizigundua mara tu baada ya mechi," alisema mtoa habari.

Alisema moja ya mikakati hiyo ni kuiondoa timu Dar es Salaam na kuipeleka Zanzibar, hivyo kubainisha kuwa mechi ya Jumamosi haitokuwa rahisi kwa Yanga kama wengi wanavyodhani.

"Mechi ile kuna baadhi ya wachezaji waliondoka kambini, hawakulala kambini kuelekea siku ya mechi, wakarejea asubuhi, lakini cha kustaajabisha, pamoja na baadhi ya wadau wa karibu kutaka wasichezeshwe kwa sababu wamekiuka miiko ya kambi, lakini walicheza na kile ndicho kilichotokea, safari hii kitu cha kwanza ni kuwaondoa mjini kwanza, mengine wanaendelea kuyafanyia kazi, kwa hiyo nakuhakikishia viongozi na wadau wengine walioletwa kuongeza nguvu wapo mzigoni, mechi haitokuwa ya kitoto kama watu wanavyodhani, tahadhari zote zimechukuliwa,"kilisema chanzo hicho.

Kwa upande wa Benchikha, amesema tatizo

INAENDELEA UKURASA 23



Wachezaji Simba wakiwa mazoezini Zanzibar

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >